# FARAGHA KWA MPANDA KANISA

## MWONGOZO KWA VIONGOZI WA WARSHA

**Maelezo**

Faragha kwa Mpanda Kanisa ni mpango wa mafunzo kwa mpanda Kanisa kufikiri juu ya vidokezo muhimu vya kuanzisha jamii mpya ya imani. Mara nyingi huendeshwa kwa siku mbili au tatu,wapanda Kanisa,mara nyingine na wenzi wao,watatafakari  vidokezo kumi tofauti kuhusiana na kuanzisha kituo kipya cha ufalme. Muda wa pamoja sio tu kwa ajili yaliyomo kwenye vipindi,bali ni kujifunza kila mtu kwa mwenzake, kutumia muda kwa maombi na marejeo na kuisikiliza sauti ya Mungu. Mtandao wa Kuzidisha unatoa Faragha hii kama fursa kwa watu kutafakari ikiwa wangependa kujihusisha zaidi na mpango wa mafunzo ya mpanda Kanisa.Tunatumaini mafunzo haya ya faragha utakuwa ni muda unaoleta uelewa na uzoefu kwa mpanda Kanisa mtarajiwa.

Mtandao wa Kuzidisha
Makanisa Mengi Zaidi, Makanisa Yenye Nguvu

Faragha kwa Mpanda Kanisa

Toleo lililosahihishwa @ 2012 na Mtandao wa Kuzidisha, Chicago, Illinoisi.
Toleo la kwanza © 2007 na Mtandao wa Kuzidisha, Chicago, Illinois na Kituo cha Mafunzo cha Kuzidisha Kanisa, Fort Wayne, Indiana.

Haki zote zimehifadhiwa. Kuzalishwa kwa masomo haya kunaruhusiwa kwa makusudi ya mafunzo. Wanafunzi wanaweza kutozwa gharama za kuchapa na gharama za tukio la mafunzo pekee. Hakuna mtu, au shirika lenye haki ya kubadilisha masomo ama kuuza nakala zilizochapishwa au za elektroniki za masomo pasipo kibali cha maandiko kutoka Mtandao wa Kuzidisha.

Nukuu zote za maandiko zimetolewa kutoka BIBLIA TAKATIFU, TAFSIRI MPYA YA KIMATAIFA (NEW INTERNATIONAL VERSION)@ Copyright © 1979, 1978, 1984 na Chama cha Biblia cha Kimataifa. Imetumiwa kwa ruhusa ya Zondervan Publishing House. Haki zote zimehifadhiwa.

**MAELEKEZO YA JUMLA**

Mwongozo wa mwalimu unabeba karibia vidokezo vyote vya kitabu cha mshiriki. Maneno yote yaliyoandikwa kwa herufi kubwa ni majibu ya nafasi zilizoachwa wazi kwenye mwongozo wa mshiriki. Mistari ya pembezoni katika miongozo yote ni kwa ajili ya kumbukumbu zako, maswali, maoni, mapendekezo, nk. Tumejitahidi kuweka kurasa zilizo sawa kwenye mwongozo wa mwalimu na wa mwanafunzi.

**Sehemu zifuatazo zinapatikana kwenye kitabu cha mwanafunzi tu:**

- **Utangulizi.** Kwa nini kupanda makanisa? Sehemu hii inaelezea dhana tatu za kitheolojia zinazohusiana moja kwa moja na upandaji kanisa: Kufanyika mwili, Missio Dei, na Ufalme wa Mungu.
- **Tathmini.** Wanafunzi wanaombwa kurejesha fomu za tathmini zilizojazwa baada ya kukamilisha faragha.
- Cheti cha kutambuliwa.

**Sehemu hizi zinapatikana kwenye mwongozo wa mwalimu tu:**

- **Maelekezo ya jumla**. Taarifa ya nyongeza na mazoezi yaliyopendekezwa.
- **Yaliyomo**
- Ratiba iliyopendekezwa kwenye kitabu cha cha mshiriki shughuli zimeorodheshwa pasipo muda/wakati.
- **Kiambatisho**
  Karatasi ya usajili. Kila mshiriki anapaswa kujaza fomu ya maombi.

**1. MAHALI**
- Utahitaji chumba cha kongamano kikubwa iwezekanavyo ili kubeba washiriki na chumba chenye uvuli wa kutosha watu kuona.
- Sharti uwe na uwezo wa kutumia ukuta kubandika kurasa za masomo zinazoonekana.
- Zaidi, mahali pawe na maeneo ambayo washiriki wanaweza kupumzika na kuburudika wakati wa vipindi vya mapumzuiko (bustani, njia, vitu vya kukalia na benchi nk).
- Pawe na sehemu za kutosha za kuchomeka vifaa vya umeme angalau vitatu kwa wakati mmoja.

**2. RATIBA**
Muda wa kuanza faragha unaweza kutofautiana, lakini ni muhimu kutoa saa 1½ kwa kila kipindi ili washiriki waweze kumaliza zoezi.

**3. MASOMO**

Kila kipindi kinaanza na makusudi yatakayotimilizwa katika kipindi hicho. Mwishoni mwa kila somo ni muhimu kuyasoma makusudi tena ili kuhakikisha yamefikiwa. Mapendekezo kwa mwalimu yanapatikana pembezoni, mkono wa kushoto wa kila ukurasa.

**4. VITU VYA LAZIMA**
Ni muhimu kuandaa vifaa vitakavyohitajika mapema:
- Kibandiko cha majina chenye majina ya kila mtu anayehusika na faragha.
- Projecta kwa ajili ya kurusha picha, au kompyuta pamoja na projekta, na skrini au ukuta mtupu/mweupe.
- Televisheni yenye mikanda ya picha/video.
- Stendi/Nguzo yenye karatasi kubwa.
- Mikrofoni na vipaza sauti.
- Utepe, notisi za kubandika, karatasi za magazeti.
- Vifaa vya sauti (kwa ajili ya kupiga muziki wakati wa mapumziko na/au kupiga muziki wa ala wakati wanafunzi wanafanya kazi za vitendo)
- Peremende /pipi, maji nk vinavyowekwa juu ya meza.
- Vyeti vya kumaliza.

**5. PROJEKTA AU PROJEKTA YA JUU**
- Kabla ya kuanza hakikisha kwamba kifaa chochote cha mawasiliano ya picha kinaweza kuonekana kwa uwazi pande zote za chumba cha kongamano. Ikiwa projekta ya juu inatumika hakikisha picha zinaonekana vizuri kwenye skrini.

**6. TATHMINI**
Kuna tathmini kwenye kitabu cha mshiriki. Hii ikamilishwe mwishoni mwa kipindi (faragha) na irejeshwe kwa viongozi wa faragha. Viongozi wanaweza kutuma muhtasari wa tathmini kwenda Mtandao wa Kuzidisha.

www.multiplicationnetwork.org

## YALIYOMO

**Kipindi cha 1 |**
Kufafanua Maono………………………………………………………… 5

**Kipindi ch 2 |**
Kubainisha Maadili ……………………………………………………… 11

**Kipindi cha 3 |**
Kubainisha Misheni ……………………………………………………… 15

**Kipindi cha 4 |**
Kujitolea Wewe Mwenyewe katika Maombi na Neno ………………… 21

**Kipindi cha 5 |**
Kujenga Timu …………………………………………………………….. 25

**Kipindi cha 6 |**
Kufanya Uinjilisti wenye Ufanisi ………………………………………… 29

**Kipindi cha 7 |**
Kupanga Kimkakati ……………………………………………………… 35

**Kipindi cha 8 |**
Kuandaa Huduma Yenye Ufanisi ……………………………………… 43

**Kipindi cha 9 |**
Kushinda Vizuizi …………………………………………………………. 49

**Kipindi cha 10 |**
Kuiangalia Familia Yako ………………………………………………… 55

**Kiambatanisho |**

i. Mafafanuzi ……………………………………………................ 61
ii. Mitindo ya Uinjilisti …………………………………………………. 65
iii. Ukarimu ……………………………………………………………….. 67
iv. Taarifa Fupi ya Mpanda Kanisa ………………………................ 69
v. ABC za Mpanda Kanisa ……………………………………………... 71
vi. Ripoti ya Mahafali …………………………………………………..72

KIPINDI CHA 1

# KUFAFANUA MAONO

**Makusudi**:

- Mshiriki ata……
- Elewa umuhimu wa kuyafafanua maono
- Jua tofauti kati ya maono na misheni
- Andika kauli ya maono au kurejea kauli ya maono iliyopo.

*"Na alipowaona makutano, akawahurumia, kwa sababu walikuwa wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji." (Mathayo 9:36).*

## A. MAANA /UFAFANUZI

*Maana rahisi ya maono ni: "Kuiangalia hatima na kuona kile ambacho Mungu anataka kukifanya kupitia kwako ili kuyatimiza makusudi yake ya ukombozi."*[1]

1. Maono ni uwezo unaotolewa na Mungu wa kuyaona mambo ambayo hayajawa, lakini yatakayokuwa **HALISI**.

2. Maono ya kanisa huamua mwelekeo na huduma zake zote. Mchakato unaanzia pale unapojisikia **KUTORIDHISHWA** Sharti pawe na namna ya kukerwa na hali halisi ilivyo. Unaiona **HATIMA** iliyo bora zaidi, wazo linalofikika ambalo tunalenga kulifanyia kazi.

3. Kuwa na maono pia ni suala la **IMANI**, kwa sababu utapaswa kushughulika na mambo ambayo huwezi kuyaona kabisa. Pasipo imani hayawezi kuwepo maono. Na kama hakuna maono, basi hakuna maisha.

4. Maono ni picha inayotia **CHANGAMOTO** na **ILIYO WAZI** ya wakati ujao wa huduma.

**Kumbuka |** Biblia inafafanua kiini cha makusudi ya Mungu kwa kanisa zima, lakini maono utakayokuwa ni maelezo maalum ya makusudi haya katika muktadha wako.

1 Wagenveld, John (ed) Sembremos Iglesias Saludables. FLET/UNILIT, 2005, 187

**Mifano michache ya kauli za maono:**

"Kanisa la Kikristo la Mfalme wa Amani linaona kusanyiko lenye nguvu na lililo hai ambalo lina wafikia watu wengi kwa injili kamili ya Yesu Kristo. Jamii hii ya imani, kama mti itakuwa na:

- *Mizizi yenye kina katika Neno.*
- *Shina lililonyooka na lililo imara ambalo ni Bwana wetu Yesu Kristo.*
- *Matawi yanayosambaa ili kuihudumia jamii na ulimwengu.*
- *Matunda yanayoakisi kujitolea kwetu wakristo.*

*Maono yatafikiwa kupitia ibada yenye nguvu, mahubiri mazito, ubora katika mafundisho ya kibiblia, huduma za kutembelea zilizo hai, uinjilisti wenye kusudi, na mkazo juu ya mahitaji ya familia na watoto katika jamii yetu."*

(Kanisa la Kikristo la Mfalme wa Amani, Puerto Rico)

"Maono yetu ni kuwa kusanyiko linalokua kikamilifu na lina nguvu katika utendaji kazi, la Kipentekoste katika roho, lenye Matengenezo katika fundisho na vitendo, na la kimataifa katika kuwafikia wengine.

(Kanisa la Kikristo la Matengenezo, Puerto Rico)

*"Kanisa katika kila jamii limepandwa na viongozi waliofunzwa, wenye ujuzi wa vitendo na waliotiwa moyo kufanya kazi pamoja.*

(Taasisi ya Wapanda Kanisa)

## B. MAONO YA BIBLIA

**Kidokezo cha Kiongozi:**

Washiriki wakae wawili wawili au katika vikundi vidogo ili kufanya zoezi hili.

Kila moja ya vifungu vifuatavyo vinatoa mfano wa maono ya Mungu yaliyofunuliwa katika Neno lake. Bainisha maono katika vifungu vifuatavyo vya kibiblia:

- Mwanzo 12: 1-3; 13:14-18

  ______________________________________________

  ______________________________________________

- 2Samweli 7:5,8, 12-16

  ______________________________________________

  ______________________________________________

- Mathayo 9:36-38

  ______________________________________________

  ______________________________________________

## C. UMUHIMU WA MAONO:

1. Yanatusaidia **KULENGA** (kujipanga) **UPYA** kwa kazi wakati mazingira yanapokubana ili ukate tamaa.

2. **YANAWAZUIA** wengine kuamua kile utakachokifanya katika muktadha wako.

3. “Pasipo maono, watu hushindwa kujizuia…. (Mith. 29:18).

**Kumbuka |** Maono yanaweza kurekebishwa na kubadilishwa kutegemeana na mazingira. Unapaswa kuwa mvumilivu, maono bado hayajawa kitu halisi.

## D. KUENDELEZA MAONO:

1. **ANDIKA** maono. Tumia msemo mfupi na rahisi ambao ni rahisi kuukumbuka ili uweze kuukariri na kuueleza vizuri.

2. **FIKIRI MAKUBWA**! Nguvu ya msukumo ni maono yaliyo wazi, ya kibiblia, yanayofikika, na yenye kutia changamoto.

3. **UWE MBUNIFU**. Jisikie huru kufikiri kwa upya, au kwa njia tofauti.

4. **CHUNGUZA** maono
   - Je, yako wazi?
   - Je, yanatia changamoto?
   - Je, yanatazamisha mbele?
   - Je, yanawezekana?

5. Shirikisha maono kwa **UWAZI** na kwa **IMANI**. Maono ya kawaida, yanayomlenga Yesu Kristo mwenyewe, yatakuwa sababu ya kuunganisha timu.
   - Weka mazingira ambayo kwayo wengine watajihusisha na maono hayo.
   - Panga timu itakayofanya kazi ili kuyafikia maono yaliyochaguliwa.
   - Unda maono makubwa vya kutosha ili kuruhusu majaribio na kushughulika na hali ya kushindwa/kutofaulu.
   - Tafuta njia mpya na za tofauti ili kuyaendeleza maono kwa kila mtu.

**Kumbuka |** Kiongozi anapaswa kushirikisha maono kwa wengine ili kupata uthibitisho wa jamii kubwa zaidi ya imani.

## E. TOFAUTI KATI YA MAONO NA MISHENI

| KAULI YA MAONO | KAULI YA MISHENI/DHAMIRA |
|---|---|
| UFAFANUZI | |
| Ni kifungu cha sentensi moja au mbili ambazo zinaelezea kwa kifupi hali ya kanisa ifaayo au ya shirika linapotimiliza kusudi lake. Kinatenda kazi kama nyota ya kaskazini ili kulifanya kanisa liendelee kwenda katika mwelekeo sahihi ili kufikia misheni/dhamira. | Ni kifungu kifupi kinachoeleza jinsi kanisa lako au shirika linavyofikia maono yake. Kinatoa "miguu na nyayo" za kufikia maono. |
| **NENO LA UFUNGUO** | |
| Nini? | Namna gani? |
| MFANO | |
| Kanisa lenye afya linawakilisha Ufalme wa Mungu katika kila jamii. | Kuwaandaa viongozi wa kanisa kwa vifaa na raslimali za kuimarisha na kuzidisha makanisa yenye afya:<br>1. Kuwafunza viongozi walezi kitaifa watakaoweza kuwafunza wapanda makanisa.<br>• Kutenda kazi pamoja na waumini wa kitaifa.<br>• Kupitia makanisa ya mahali pamoja<br>• Tunapo "wafunza wakufunzi"<br>2. Kutoa nyenzo zinazozalishika. Kuunda vitabu vya masomo, vitabu vya kazi, na kozi za mafunzo zinazoweza kutolewa na kutumiwa bure katika ulimwengu.<br>• Kutumia ofisi zinazoonekana<br>• Kukuza matumizi ya teknolojia. |



## POINTI ZA VITENDO

1. Ikiwa Mungu angetenda katika huduma pasipo kipingamizi, je, Kanisa lako lingekuaje kwa miaka kumi ijayo?

2. Andika maono yako, kwa kifupi

3. Pima maono yako dhidi ya miongozo ya sehemu D iliyopo juu ("Kuendeleza Maono"). Je, maono yako yanaweza kufafanuliwa kwa uwazi? Je, yanatoa taswira ya hatima inayotamaniwa? Kama ni lazima, andika tena maono yako. Yawe wazi, rahisi na yanayolenga kitu muhimu/pointi.

4. Chukua dakika chache kushirikisha maono yako kwa ushiriki mwingine ama kundi zima.

KIPINDI CHA 2

# KUBAINISHA MAADILI

*“Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao…” (2Tim. 3:14).*

## A. UFAFANUZI

1. Maadili ni taratibu/sheria za **MWENENDO** na mitazamo ambaye kwayo tunaishi.
2. Maadili yetu yanadhihirishwa kupitia **MATENDO** fulani mahususi.
3. Maadili sio **MAFUNDISHO** ya mfumo wa imani.
4. Maadili yanatoa **MSINGI** ambao kwa huo kanisa litaweka malengo.

Kumbuka |Misheni haiwezi kuhitilafiana na maadili ya mpanda kanisa, kwa hakika, misheni husimama kutokana na maadili.

## B. MAADILI YA KIBIBLIA NA MAADILI YA MSINGI YA SHIRIKA

Maadili ya Kibiblia sio kanuni zisizoweza kujadiliwa ambazo zinaeleza sura na kuamua mfumo wa maisha ya mkristo. Katika makundi ya watu wawili au watatu, angalieni vifungu vifuatavyo vya Kibiblia na kubainisha maadili yaliyotajwa.

Kutoka 3:7-10

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

Mathayo 18:10-14

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

**Makusudi:**

Washiriki wata…..

- Elewa umuhimu wa kuanzisha maadili.
- Kuainisha maadili ya shirika lake.
- Kuunda orodha ya maadili na kujadili namna yatakavyotekelezwa.



**Zoezi linalowezekana:**

Washiriki wanaweza kujadili hali ya kufikirika ya kanisa inayodai kuwa na maadili ya uinjilisti.

Waulize “Je, utauliza swali gani ili kujua kama kanisa kweli linajali

1Wakorintho 1:10

2Timotheo 3:14

Kwa nyongeza ya maadili ya kibiblia, mpanda kanisa anapaswa vile vile kuelezea maadili ya msingi ya shirika lake.

Maadili haya yatapimwa kwa makusudi ya kanisa jipya na yatahusisha muktadha kwenye maelezo.

*"Kila tendo linalochukuliwa na shirika lazima liunganike na maadili, yaliyowekewa vipaumbele. Kwa kila moja ya maadili ya msingi, shirika ni sharti likamilishe sentensi ifuatayo:* "Tutajua kwamba tunaishi chini ya maadili haya wakati…[1]"

*"Maadili mazuri ni ya kibiblia, yanaumba shauku, yanashirikishwa kwa wengine, ni ya kuendelea/endelevu, yanaweza kuelezwa kwa uwazi, yanakubaliana na maadili mengine, na yanaweza kutekelezeka"[2].*

Kama mfano, yafuatayo ni maadili ya msingi ya Mtandao wa Kuzidisha:

- **UADILIFU WA MKRISTO**
  Tunalenga kutii mafundisho ya Yesu Kristo kama yalivyofundishwa katika maandiko kwa mazingira ya uanafunzi na neema (Waefeso 4).

- **UONGOZI WA TIMU**
  Tunalenga kuwatumikia wengine tukimtegemea Roho wa Kristo, tukikuza karama na michango ya washiriki wote wa timu (Wafilipi 2).

1. Blanchard, Ken and Hodges, Phil. Lead Like Jesus. Thomas Nelson, 2005
2. Malphurs, Aubrey Value. Driven Leadership. Baker Books, 1996.



Matendo. 2:42- 47

- **UBORA KWA NYENZO NA MAFUNZO**
  Tunalenga kuzalisha nyenzo bora za mafunzo na kuendesha matukio ya mafunzo rasmi ambayo yanaweza kuelezwa kuwa ni ya kiwango cha juu cha ubora (Waefeso 6:6-8).

- **KUZALISHIKA NA KUFIKIWA KWA URAHISI**
  Tunalenga kwamba nyenzo za mafunzo na mafunzo yafikiwe na wote wanaopenda kuyatumia, kupitia tovuti ambayo ni rahisi kuitembelea na kupitia upanuzi endelevu wa kijiografia wa viongozi wa kuzidisha (2Timotheo 2:2).

- **UWAKILI UNAOWAJIBIKA**
  Tunalenga kutoa uwajibikaji makini na uwazi kwa huduma yetu mbele za Mungu na wengine, tukiwa wasimamizi wazuri wa raslimali na fedha za huduma (1Nyakati 20:10-14).

## C. UMUHIMU WA MAADILI

1. Mara nyingi migogoro huibuka makanisani kwa sababu ya **MATARAJIO** tofauti.

3. Jitihada nyingi za mipango mkakati hazifaulu kwa sababu maadili hayakubainishwa **MWANZONI** mwa mchakato.

**Kumbuka |** Ikiwa maadili katika kikundi yatatofautiana kimsingi, hakuna mpango wa kazi unaoweza kutekelezwa kwa ufanisi. Pasipo maadili yanayoelezeka na kukubaliwa na wote, hakutakuwa na umoja ndani ya kanisa.

## POINTI ZA VITENDO

1. Tengeneza orodha ya maadili makuu ya kibiblia. Ni kwa njia zipi maadili haya yapo kwenye kanisa jipya? Waombe washiriki kuyaweka pamoja maadili yanayofanana.

2. Weka orodha ya maadili ya msingi yanayowezekana. Hakikisha kwamba maadili haya yanaakisi vitendo mahususi.

3. Panga orodha kwa utaratibu wa kipaumbele. Elezea kila moja ya maadili kwa mifano thabiti ya tabia. Waombe washiriki waandike maadili yasiyozidi saba.
   a. 
   b. 
   c. 
   d. 
   e. 
   f. 
   g. 

# KUBAINISHA MISHENI/DHAMIRA

*Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu…" Mathayo 28:19 (NIV)*

## A. UFAFANUZI

*"Kauli ya Misheni/Dhamira inatueleza **JINSI** shirika lako linavyofanikisha maono yake. Inaweka "miguu na nyayo kwenye maono…"*
Renee N. Hale, Missio Dei partners.

## B. VIDOKEZO

Kauli ya misheni sharti ijibu maswali matatu:

**1. Je, unamhudumia nani?**
Unahitaji kufikiria tabia zifuatazo kwa watu unaolenga kuwahudumia.

- Umri
- Kiwango cha kipato
- Ukubwa wa familia
- Kabila na asili ya utaifa
- Kiwango cha maandalizi ya kitaaluma
- Aina za shughuli/kazi
- Familia na makundi ya jamii
- Vitu wanavyopendelea na shughuli za jamii

Unapaswa kufikiri pia asilimia ya makundi tofauti kwa takwimu za watu unaowalenga, kama vile:

- Hana mwenzi, ana mwenzi, wazazi wasio na wenzi, wajane, waliotalikiwa.
- Familia ambazo wanandoa wote wanafanya kazi nje ya nyumbani dhidi ya ndoa ambayo mmoja anafanya kazi.
- Wanaomiliki nyumba kinyume na wanaopanga.

**Makusudi:**

Mshiriki ata……

- Elewa umuhimu wa kuelezea dhamira.
- Fahamu tofauti kati ya maono na misheni.
- Andika kauli ya misheni au kurejea kauli ya maono iliyopo.

Mshiriki ata…….

- Elewa umuhimu wa kuwa na kauli ya dhamira ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kanisa lao au shirika.

- Andika kauli ya dhamira.

**Kidokezo cha kiongozi:**

Hiki ni kielelezo cha mapitio ambacho kinaweza kutumiwa ili kukielewa kikundi chako lengwa na mahitaji yake.

- Je, wewe ni mshirika hai wa kanisa la mahali pamoja?
- Je, unaamini ni mahitaji gani makubwa katika jamii hii?
- Unafikiri kwa nini watu wengi hawaendi kanisani?
- Kama ungekuwa unatafuta kanisa katika eneo hili, je ungefuatilia mambo yapi?
- Ungenipa ushauri upi mimi kama mchungaji wa kanisa la mahali?
- Je, ningeliweza kukufanyia nini?
- Je, unavutiwa kusikia habari zaidi kuhusu kanisa letu?

**Dhamira ya kanisa ni ya kipekee:**

Makanisa mawili hayawezi kuwa na kauli ya dhamira inayofanana kwa sababu majibu ya maswali matatu ya msingi yatakuwa ya tofauti kwa kila hali.

Hii inaruhusu uwepo wa makanisa mawili au matatu katika jamii, kila moja likiwa na huduma tofauti, likiwafikia watu tofauti na kukutana na mahitaji tofauti.

Swali hili lazima lifuatiwe na mengine:

- Ni Habari Njema ipi kwa watu unaotaka kuwafikia?
- Ni mahitaji gani ambayo kanisa lako peke yake litayatimiza?.

3. Ni jinsi gani unaweza **KUTIMIZA** misheni yako?

Jibu swali hili kwa:

- Kueleza mikakati ili kuvutia kikundi chako lengwa.
- Kubainisha aina za huduma zitakazotosheleza mahitaji ya kikundi hiki.
- Kufafanua jinsi kanisa litakavyowajadili na kuzidisha wanafunzi wake kwa kuamua ni lini wataanza.

**Mifano ya Kauli ya Dhamira /Misheni**

*“Dhamira ya Vida Cristiana ni kuwahudumia mwili wa Kristo unaotumia Lugha ya Kihispaniola kwa kupitia uongozi wa kinabii, mafundisho husika na habari za yale ambayo Roho Mtakatifu anayafanya katika ulimwengu ili kutusaidia kuwa wajenzi wa madaraja katika jamii ya kimataifa.”*
(Tangazo lililoonekana kwenye jarida la Charisma).

*"Huduma yetu ya Kihispania ipo ili kuyaandaa makanisa ya Kihispania kuwatafuta waliopotea na kufanya wanafunzi wapya katika vizazi vyote kupitia ushauri, machapisho na raslimali"* (Christian Reformed Church of North America).

*“Kanisa (letu) lipo ili kuimarisha familia za Kihispania zilizoko maeneo ya Tacoma, Washington kiroho, kihisia, kiakili, na kimwili, kuwaandaa kwa maendeleo ya kiroho katika mazingira ya imani"* (The Rock Church, Open Bible Church).



2. Je, ni **MAHITAJI** yapi ya kushughulikia?

## C. BIBLIA NA DHAMIRA YA KANISA

Rejea vifungu hivi kutoka kwenye maandiko yanayoeleza kusudi la kanisa.

Luka 24:46 - 48

______________________________________________

______________________________________________

Matendo 2:42 - 47

______________________________________________

______________________________________________

Wagalatia 6:10

______________________________________________

______________________________________________

Waefeso 4:3 - 4

______________________________________________

______________________________________________

1Yohana 2:3-6

______________________________________________

______________________________________________

## D. KWA NINI KAULI YA DHAMIRA NI MUHIMU?

1. Nini kitatokea ikiwa dhamira ya kanisa haijaelezwa kwa uwazi?

- Kupoteza **LENGO**
- **KUCHANGANYIKIWA** daima juu ya nini kinapaswa kufanyika.
- **KUVUNJIKA MOYO** kwamba kanisa halisongi mbele kufikia maono
- **KUTOKUKUBALIANA** zaidi kati ya washiriki wa timu ya Uongozi.

1 KIPINDI CHA 3

LENGO – KUCHANGANYIKIWA – KUVUNJIKA MOYO – KUTOKUKUBALIANA



**Viongozi:**

Waulize washiriki kukamilisha zoezi wakiwa wawili wawili au vikundi vidogo.

- Majukumu yana **MUUNGANIKO** vizuri na MAONO/lengo.
- Viongozi wanaelewa kinachohitajika kufanyika, **HAWAPOTEZI** muda kwa mambo yasiyo ya msingi.
- Viongozi hawagongani mara kwa mara juu kile kinachopaswa kufanyika.
- Majukumu yasiyoongoza kwenye maono yanaweza **KUONDOLEWA**.

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

## E. KUTUMIA KAULI ZAKO ZA DHAMIRA NA MAONO

1. Jifunze na **UKARIRI** kauli ya maono na kauli ya dhamira, na wape motisha timu yako wafanye vivyo hivyo.

2. **PANGA** kauli na kuzibandika kwenye ukuta wa ofisi, nyumbani na kanisani.

3. **ZIINGIZE** kwenye kitabu cha shughuli za kanisa.

4. **ZIRUDIE** tena na tena mpaka zitakapozama ndani ya kila mtu kwenye timu ya huduma.

5. **ZIPITIE** mara kwa mara ili kuhakikisha uko kwenye njia inayotakiwa.

MUUNGANIKO – HAWAPOTEZI – KUONDOLEWA – UKARIRI – PANGA – ZIINGIZE – ZIRUDIE - ZIPITIE



3. Manufaa ya Kauli ya Dhamira

## POINTI ZA VITENDO

1. Andika sentensi moja ya jibu la swali, “Kwa nini kanisa liko hapa?"

2. Andika kauli yako ya dhamira kwa kuorodhesha a) nani unalenga kumfikia kwa injili, na b) kazi ambazo kanisa lako litazitekeleza ili kufanya maono yatokee (pamoja na Baraka za Mungu).

3. Tathmini kauli yako ya dhamira kwa kuuliza maswali yafuatayo:

    a) Je, inabainisha kikundi chako cha huduma kinacholengwa?
    [Ikiwa mmeshabainisha kikundi chenu mnacholenga, ni wakati mwafaka kabisa wa kuchambua kile mnachokifahamu hasa kuhusiana na kikundi hicho]
    b) Je, inaweka wazi mahitaji ambayo huduma yako inalenga kuyatimiza?
    c) Je, inaendana na maandiko yanafundisha? Je, ni ya kudumu? Ni fupi? Inaweza kukaririwa? (ikiwa lazima iandike tena kauli ya dhamira ili kuvifikia vigezo hivi).

4. Andaa kauli mbiu inayofupisha kauli ya dhamira kwa maneno matano hadi kumi.

5. Orodhesha njia kadhaa za kuielezea kauli yako ya dhamira.

KIPINDI CHA 4

# KUJITOA BINAFSI KATIKA MAOMBI NA NENO

*“Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani; mkituombea na sisi pia, kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake, tuinene siri ya Kristo, ambapo kwa ajili yake numefungwa” Wakolosai 4:2-3*

*“… tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema. 2Timotheo 3:15.*

**Ukweli wa Mungu unapatikana katika Biblia.**

Mungu amechagua **KUWASILIANA** na mwanadamu na kuyajulisha mapenzi yake kupitia Neno lake.

*“Maombi siyo kujiandaa na vita. Maombi ni vita”*

*“Biblia ni chakula cha wanamieleka…’ Sio kwa ajili ya wale tu wanaokutana kwenye miduara ya wacha Mungu kwa ajili ya kujengana, bali kwa ajili ya wale waliojihusisha katika mapambano ya maombi na mapigano ya imani katika ulimwengu. Biblia peke yake kama ndio mwisho itakuwa butu. Hata hivyo, wale wanaojihusisha katika mapambano yoyote wanahitaji chakula kinachong’enywa na chenye virutubisho. Si wingi wa chakula tunachokula, wala sio wingi wa maarifa ya Biblia tunaoupata ambao unatulisha, bali ni kiwango cha chakula kinachomeng’enywa.”*

**Makusudi:**

Washiriki wata…..

- Jadili utendaji wao wa sasa katika maombi na kujifunza Biblia.
- Bainisha maeneo yao ya ukuaji katika maombi na kujifunza Biblia.

1. Weber, Hansi – Ruebi The Books that reads me, WCC Publications, 1995

**Kwa habari ya njia za kuomba katika kundi, tunatoa mashauri yafuatayo:**

- Baada ya muda wa kuuliza mahitaji maalum, watie moyo washirika kuwaombea mtu aliye mkono wao wa kuume au wa kushoto, ili kila mtu aweze kumwombea mwingine.
- Mweke mtu mwenye mahitaji maalum katikati ya duara, na wengine wamwombee.
- Chukua dakika 5 hadi 10 kuandika maombi na kisha uyasome.

Wakati wa sala na maombi, watie moyo watu kujinufaisha na nyakati za ukimya na kuzitumia kama nafasi ya kutafakari na kumshukuru Mungu.

## A. WAJIBU WA MPANDA KANISA

1. Jitoe mwenyewe katika **MAENDELEO YA KIROHO** ya kikundi cha msingi.

   a. Hakikisha kwamba maombi na kusoma Biblia ni sehemu muhimu za maisha ya kila mshirika.
   b. Sisitiza kila mshirika aombe kila siku kwa ajili ya mtu asiyeamini (ambaye si Mkristo).

2. **WAPE HAMASA timu yako kwa mafunzo ya Biblia**

   a. Uwe mfano wa mafunzo ya Kibiblia endelevu kupitia ama elimu rasmi au kazi binafsi za kujifunza Biblia.
   b. Tafuta njia za kushiriki kikamilifu kwenye mafunzo ya kibiblia ya kikundi chako cha msingi.
      - Waeleze kuhusu fursa za mafunzo.
      - Kutoa msaada wa kiuchumi kwa ajili ya mafunzo.
      - Chukua muda kuzungumzia wanachojifunza.

3. **Hamasisha timu ya WAOMBEZI**

   a. Tengeneza orodha ya watu wanaovutiwa na uwaalike kujiunga na timu yako ya maombezi.
   b. Ombea waombezi wako angalau mara moja kwa juma
   c. Ungana nao kibinafsi angalau mara kwa mwezi ili kuwatia moyo, kuwashirikisha majibu ya maombi na mahitaji maalumu na kuchunguza kama ni kweli wanaomba au ikiwa utapaswa kutafuta wengine.

4. **Maombi yaendelee kuwa kiini:**

   a. **MIFANO** iliyopo ya maombi kwenye kanisa jipya.
      - Kwenye ibada za kanisa, maombi yawe rahisi, yanayoeleweka na yaliyojaa imani.
      - Omba kwa kutumia hatua za maombi (ABC za maombi: Ya kusikika, Ya kifupi, Yenye kiini katika Kristo.

---
2 Imetolewa kutoka Pfaff, Nancy – Church Resources Ministries Reno, NV

b. Mara zote sherehekea **MAJIBU** ya maombi. Hakuna kitu kinachotia moyo zaidi kama kuona jinsi Mungu anavyojibu maombi yako. Unaposherekea, uwe mbunifu, mwenye shukrani, na mnyenyekevu.

**Kumbuka |** Hakuna njia moja sahihi ya kuomba. Uwe mbunifu unapoomba. Kumbuka pia kuomba polepole, ukichagua maneno yako kwa umakini, na kuwa na ufahamu wa yale unayosema. Hii itakusaidia kuepuka kutumia majina ya Mungu kama "magongo" wakati wa maombi na itaruhusu mfumo wa maombi wenye mazungumzo zaidi.

**B. MATOKEO YA MAOMBI NA KUJIFUNZA BIBLIA**

Soma vifungu vifuatavyo na uainishe yale anayofanya Mungu wakati tunapoomba na kujifunza Neno lake.

Yoshua 1:8

______________________________________________

______________________________________________

Zaburi 40:1-3

______________________________________________

______________________________________________

Mathayo 4:3-4

______________________________________________

______________________________________________

Mathayo 7:7-11

______________________________________________

______________________________________________

Wafilipi 1:9-11

______________________________________________

______________________________________________

**POINTI ZA VITENDO**

1. Weka orodha ya kanuni za maadili ya kibiblia. Ni kwa njia zipi maadili haya yanakuwepo katika kanisa jipya? Waombe washiriki wayaweke pamoja maadili yanayofanana.

2. Tengeneza orodha ya maadili ya msingi yanayowezekana. Hakikisha kwamba maadili haya yanaakisi tendo mahsusi.

3. Ipange orodha kulingana na mtiririko wa kipaumbele. Elezea kila moja kwa mifano yenye nguvu ya tabia. Waulize washiriki kuandika maadili yasiyozidi saba.
   a.
   b.
   c.
   d.
   e.
   f.
   g.

KIPINDI CHA 5
# KUJENGA TIMU

*"...siku zote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza Injili…"*
*Wafilipi 1:4-5*

*"… kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi…"*
*1Korintho 12:14*

## A. UMUHIMU WA KUJENGA TIMU

Viini vya mwili wa mwanadamu vinajizalisha au vinakufa. Kwa njia hiyo hiyo, ndani ya kanisa la Kristo, ikiwa hautakuza wanafunzi na kuwahusisha wengine katika huduma, haitakua.

Hakuna mchungaji anayeweza kufanya kazi zote muhimu katika kuanzisha kanisa. Kujaribu kufanya kila kitu peke yako kutakusababishia uchovu kwa upande wako na kuvunjika moyo kwa upande wa wengine ambao karama zao hazitumiwi.

Baada ya kuwa umefafanua maono, umebainisha dhamira yako na kuweka wazi maadili yako, hatua inayofuata ni kukifunza kikundi chako cha msingi kuanzisha kanisa. (Kwa njia nyingine kikundi cha msingi kitaacha kanisa moja na kuanzisha lingine). Kisha kikundi cha msingi kitashughulikia maono, dhamira na maadili kwa pamoja).

Kuna njia kadhaa za kuwaandaa na kuwafunza watu kujiunga nawe katika kuanzisha kanisa jipya. Uzuri wake, watu unaowahubiri injili watakuwa wanafunzi wa sehemu ya uongozi wa kikundi cha msingi vile vile unaweza kuwaandaa wengine wawe sehemu ya kikundi chako cha msingi. Nyote kwa pamoja mtaanzisha kanisa jipya.

## B. VITENDO VILIVYO BORA KATIKA KUANZISHA TIMU

1. Hakikisha **MAONO**, **DHAMIRA** na **MAADILI** yameelezewa na yako katika maandishi na kwamba watu katika timu wanayaelewa, kukubaliana nayo. Pitia maono, dhamira na maadili mara kwa mara ili kuhakikisha maamuzi yanafanywa kwa kuyazingatia na kwamba mnatembea kuyaelekea maono.

**Makusudi**:

Washiriki wata….

- Elewa umuhimu wa kufanya kazi katika timu.
- Kuwa makini juu vitendo bora vya uongozi.
- Rejea uzoefu wao wa awali katika kuongoza timu na kuamua hatua zinazofuata katika kuandaa timu

2. **SHIRIKISHA** huduma kama timu. Ombeni pamoja na kujadili mikakati kwa kazi tofauti za huduma (kufuatilia Wakristo wapya, kujihusisha na watu ambao si Wakristo, n.k).

3. B**AINISHA**.Bainisha karama za kila mtu katika timu.Bainisha uwezo wao na maeneo wanayohitaji kukua. Wape majukumu yanayoendana na karama za washiriki wa timu.

4. Wape wanatimu wako wajibu unaoongezeka viwango. Hii itawaandaa kushika majukumu kwa wakati ujao.

5. Endelea **KUWATIA** moyo timu yako na wape mkono pale inapohitajika. Washukuru na wasifie hadharani (mbele ya watu) na wakiwa peke yao.

6. **WAFUNZE** timu yako mtu mmoja mmoja na katika vikundi.Katika kuanzisha Kanisa kutenga muda wa kuwafunza viongozi inafaa kwa mafanikio ya Kanisa.Wasaidie washiriki wa timu kushughulikia udhaifu wao mmoja mmoja kwa wakati - sio wote kwa mara moja.

7. Huku ni muhimu kwa mwenzi wako kuunga mkono Kanisa jipya na kutumia karama zake ili kusaidia likue, tunapendekeza kwamba mwenzi asiwe sehemu ya kikundi cha Uongozi. Hii itakusaidia kuweka mipaka yenye afya kati ya huduma na maisha yako ya nyumbani. Katika baadhi ya mazingira inafaa.

8. **WASILIANA**, Wasiliana, wasiliana. Tumia muda kuzungumza na timu yote, vilevile na kila mshiriki mmoja mmoja Waache wajue kwamba unapatikana pale jambo au hitaji linapotokea.

**C. KUSHUGHULIKA NA MATATIZO:-**

1. Unapoomba watu kuwa sehemu ya timu na hawawezi kufanya hivyo kwa wakati huo, kumbuka kwamba “hapana” inaweza kuwa “BADO”

2. Unapokabiliana na uamuzi mgumu, kwanza wanatimu **WAOMBE** pamoja kisha rejeeni maono, dhamira na maadili ili kwamba uamuzi ufanyike na wao wakifahamu.

3. **SULUHISHA** migogoro mara tu unapoigundua. Wape watu fursa kujieleza na uhakikishe watu wanasikilizana kwa umakini.Uweke mtindo mzuri wa kusikilizana.

4. Usiahidi kitu usichoweza kukitimiza/kutoa. Ukiona kuna kitu ulishasema ungekifanya, lakini hujaweza kufanya, uwe mkweli, na uombe msamaha mara moja.

## D. TABIA NANE ZA TIMU ZENYE MAFANIKIO[1]

Timu zenye mafanikio zina………

1. **MALENGO** yaliyo wazi na ya kuvutia. Wakati kila mtu anapotenda kazi kwa kufuata lengo linalofahamika, nguvu za wanatimu huongezeka na makusudi ya kawaida ya timu yanaimarishwa.

2. **MUUNDO** uliopangiliwa ili kufikia matokeo. Timu lazima ipangiliwe kwa namna ambayo itawezesha mafanikio.

3. Washiriki wa timu wenye **UWEZO**. Timu yenye washiriki ina watu wanaojua wajibu wao na kazi yao sawasawa.

4. Kujitolea kwa njia ya **KUSHIRIKIANA** kwa washiriki na timu. Washirika na timu wanaelewa kwamba mara nyingine wanapaswa kuidhabihu mivuto yao kwa faida ya timu.

5. Mazingira ya **MSHIKAMANO**. Mazingira ya kufanyia kazi yainue mawasiliano mazuri na shauku ya kushirikiana.

6. Kiwango cha **UBORA**.Timu zenye nguvu, zenye ufanisi haziridhishwi na hali ilivyo. Wanalenga ubora katika kazi yao.

7. Msaada wa nje na **KUTAMBULIWA**. Timu zinazoungwa mkono na uthibitisho kutoka kwa wengine wanaelekea kufanya vizuri zaidi katika kufikia malengo yao.

8. Uongozi unaoendeshwa na **KANUNI.** Viongozi wanapofanya maamuzi yanayolenga kanuni zilizokubaliwa kwa pamoja, wanaongeza ujasiri na timu inafanya kazi.

1Larson, Carl ans Frank Lafasto. *Teamwork: What must Go Right/What can Go wrong* Sage Publications, 1989.

## POINTI ZA VITENDO

Katika makundi ya watu watatu au wanne, fanyeni yafuatayo:-

1. Orodhesheni mambo yanayozuia mafanikio ya kazi ya timu

2. Toa mfano wa wakati :-
   - Ulipowahusisha wengine kufanya uamuzi
   - Ulipompa fursa mtu mwingine kutumia karama katika huduma
   - Unapowasaidia watu kutatua mgogoro
   - Hukuongoza kikundi vizuri – nini kilitokea?

3. Ni hatua mbili zipi zinazofuata unazohitaji kuzichukua ili kuendeleza timu yako ya Uongozi?

   a.

   b.

**KIPINDI CHA 6**

# KUFANYA UINJILISTI WENYE UFANISI

*"Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakihubiri Neno" Matendo 8:4*

## A. KUJITOA KWENYE UINJILISTI

Amri ya mwisho ambayo Kristo alitupa kabla ya kupaa Mbinguni – *"Enendeni mkawafanye Mataifa yote kuwa Wanafunzi"* (Mathayo 28;19)-iwe kipaumbele kwa kila Kanisa. Katika mchakato wa kufanya Wanafunzi kama Mtume Paulo alivyosema mtu mmoja anapanda na mwingine humwagilia, bali Mungu ndiye akuzaye (1 Kor.3:6-7) Hivi bado inaonekana mtu mmoja anatoa ujumbe wa injili wa kwanza wakati wengine hufuatilia kwa maelezo zaidi na majibu kwa maswali bali Mungu anaendelea kuwa mwenye kubadilisha mioyo na kuongeza watu katika familia yake. Kanisa bado ni chombo ambacho Mungu anakitumia kuwatafuta waliopotea na kuwafundisha.

Mtume Paulo anarejea kwa waliochaguliwa, ambao Mungu aliwaita kabla ya kuwepo kwa Ulimwengu (Efe. 1:4) Kwa kuwa hatujui waliochaguliwa ni akina nani, tuhubiri habari njema kwa Ulimwengu wote tukijua kwamba Mungu atatenda kazi katika maisha yao akiwafanya kuitikia vyema Injili. Sisi ni vyombo vya Mungu katika mchakato huu tukienda na kuwafanya Wanafunzi katika mataifa yote.

Kwa sababu Mungu yuko kazini makanisa yanaweza kutazamia **UKUAJI**-watu wengi zaidi wanamjia na kumjua Yesu kuwa Mwokozi na kuishi kwa kumtii yeye. Inasikitisha kwamba kuna makanisa mengi ambayo matazamio yao yako chini sana kiasi kwamba wanafanikisha: kwa urahisi hawakui.

**Makusudi washiriki wata…………..**

- Jifunze kanuni za ufunguo za kufanya Uinjilisti wenye ufanisi.
- Elewa hadhira/wasikilizaji wao na njia za kuwafikia kwa injili.
- Ainisha mitindo ya uinjilisti binafsi wanayoipendelea.

## B. KANUNI ZA UFUNGUO KWA UINJILISTI

- Toka nje na kuwatafuta waliopotea (usiwasubiri wao waje kwako)
- Thamini kile ambacho Mungu anakithamini.
- Jali wahitaji wa kiroho.
- Iga mbinu, sio Ujumbe.

1 Malphurs, Aubrey Planting Crowing Churches for the 21st Century. Baker Book House, 1998

- Tafuta ardhi yenye rutuba ili kupanda ujumbe (kutafuta watu walioandaliwa na Roho Mtakatifu)
- Kuwasiliisha Injili kwa uwazi kwa njia zinazoleta maana
- Kuvua kwa kutumia ndoano nyingi- kushirikisha Injili kwa watu wengi kwa njia nyingi - kupitia maneno, matendo, aina mbalimbali za matukio n.k.
- Kusindikiza Uinjilisti kwa maombi.
- Kutafuta Wanafunzi, sio maamuzi tu.
- Kufanya kazi kupitia mahusiano yaliyopo na ya asili

**C. LENGA WASIKILIZAJI (HADHIRA**)

Lenga kufikia kikundi maalumu cha watu kwa Uinjilisti. Hii ni kanuni ya Kibiblia na ya vitendo. Kama vile Mungu alivyofanyika mwili katika Utu wa Yesu ili **KUJITAMBULISHA** kwa wanadamu hivyo kupitia Kanisa (mwili wa Kristo) Yesu anavaa Mwili katika jamii fulani, akijihusuisha na mahitaji yake na kuiletea Injili kamilifu.

Baadhi ya watu wanakataa wazo la kulenga kikundi maalumu. Hata hivyo, mtume Petro na Paulo walifanya hivyo.Mmoja akitoka kuwa Mmishionari kwa Wayahudi na mwingine kuwa mmisionari kwa Mataifa na pamoja na kuwa hawakumbagua mtu walipokuwa wakihubiri Injili, ni ukweli pia kwamba walikuwa wakijaribu kuwafikia wasikilizaji maalumu.
Kuwa na kikundi lengwa kinachoelezwa kwa uwazi kunarahisisha zaidi kufanya maamuzi ya jinsi ya kuitekeleza huduma.

Rudi nyuma kwenye kauli ya dhamira uliyoandika kwenye kipindi cha tatu (Uk.19).Ni vikundi gani unatafuta kuvifikia kwa Injili.

Ni njia zipi zitakuwa zenye ufanisi kuishirikisha Injili kwao?

Ni njia zipi za kufanya uinjilisti ambazo yawezekana hazitafanya kazi kwa kundi hili la watu?

**D. KUPANGA KWA AJILI YA UINJILISTI**

Kazi kubwa ya wale wanaoanzisha Kanisa jipya, hasa mwanzoni sharti iwe Uinjilisti.Makanisa imara yana nia na Uinjilisti na wanaendeleza lengo hili kwa mipango endelevu ya Uinjilisti. Ili Uinjilisti uwe kipaumbele, unahitajika uwe sehemu ya mpango. Hakikisha kuwa kuna **BAJETI** kwa ajili ya shughuli za Uinjilisti na ziwekwe kwenye **KALENDA.** Kuwashirikisha watu habari njema sio kitu kinachotokea mara moja moja.

**E. MITINDO BINAFSI YA UINJILISTI**

Tunapojadiliana juu ya muktadha na kuanzisha makanisa mapya, watu wanashangaa; Ni njia ipi iliyo bora kwa ajili ya kuhubiri Injili? Ipi inayoleta matokeo yaliyo bora?
Tutumie mbinu ipi?
Ukweli ni kwamba hakuna kanuni ya ajabu inayosuluhisha changamoto zetu zote za Uinjilisti. Wale wanaoanzisha Kanisa sharti watafute mbinu zifaazo na kuziweka katika matendo.

Tunapendekeza upitie mitindo ya Uinjilisti ifuatayo na kwamba uwatie moyo watu katika timu yako ya Uongozi kupitia pia. Tafuta njia za kulinganisha mbinu zitakazofaa zaidi kwa wasikilizaji wako na kwako na mitindo inayopendelewa na timu yako ya Uinjilisti.

Kumbuka| Muda ukiruhusu na ikiwa Kiongozi wa warsha atakuambia ufanye hivyo, soma pointi D za Kidokezo cha1: Uinjilisti

BAJETI - KALENDA

## MAPITIO YA MITINDO YA UINJILISTI

Andika majibu yako kwa kila moja ya maelezo yote 36, kutegemea na jinsi yanavyofanya kazi kwako binafsi (yanavyokufaa).

**1= HAKUNA   2= KIDOGO SANA   3= KIDOGO   4= SANA**

| | |
|---|---|
| 1. | Kwenye mazungumzo, ninapenda kwenda kwenye mada moja kwa moja, pasipo kuzungumza mno au kufanya mazungumzo madogo madogo. |
| 2. | Napata wakati mgumu kuondoka stoo ya vitabu au maktaba pasipo lundo la vitabu ambavyo vinanisaidia kuelewa mada ambayo jamii inabishania. |
| 3. | Mara nyingi ninashirikisha hadithi za uzoefu wangu binafsi ili kufafanua pointi ninayojaribu kuiwasilisha/ kuieleza. |
| 4. | Ni mtu ninayewapenda sana watu, ninathamini sana urafiki. |
| 5. | Ninafurahia kuwahusisha au kuongeza watu wapya kwenye shughuli ninazofanya |
| 6. | Ninaona mahitaji katika maisha ya watu ambayo wengine mara nyingi hawayaoni. |
| 7. | Siogopi kuwaweka watu mahali pao ikiwa ni lazima. |
| 8. | Napenda kuchambua mambo. |
| 9. | Mara nyingi ninajihushisha na watu wengine kwa kutumia maneno kama vile “Nilifikiri hivyo hivyo” au “Nimejisikia hivyo hivyo”. |
| 10. | Baadhi ya watu wametoa maoni juu ya uwezo wangu wa kuongeza marafiki wapya. |
| 11. | Kuwa mkweli, hata pale ninapojua majibu, ninajisikia raha mtu fulani mwenye sifa zinazostahili zaidi yangu anapoueleza Ukristo kwa marafiki zangu. |
| 12. | Ninajisikia kuridhishwa zaidi ninaposaidia wengine ikiwa si kitu kinachofanya mbele ya watu (Hadharani) |
| 13. | Sioni shida kukabiliana na marafiki zangu na ukweli hata kama itaonekana kuhatarisha uhusiano. |
| 14. | Kwa kawaida ninalenga mazungumzo yanayohusu maendeleo ya watu, kukosekana kwa maendeleo katika maisha yao ya kiroho. |
| 15. | Ninapowaambia watu jinsi nilivyokuwa / nilivyofanyika mkristo, ninagundua kwamba wanavutiwa. |
| 16. | Ninapendelea kujadili mambo ya binafsi kuliko dhana za kitheolojia. |
| 17. | Ninapojua juu ya tukio muhimu la kiinjilisti ambalo marafiki zangu watalifurahia, ninafanya kila jitihada kuwaalika. |
| 18. | Ninapendelea kuonyesha upendo wangu kupitia matendo kuliko maneno. |

| | |
|---|---|
| 19 | Ninaamini kuwa upendo wa kweli mara nyingi inamaanisha kumwambia mtu ukweli hata kama unauma. |
| 20. | Ninafurahia kujadiliana na kuhojiana maswali magumu. |
| 21. | Ninawaeleza wengi makosa yangu, hasa pale yanaponisaidia kuyahusianisha na majibu/ suluhisho nililopata |
| 22. | Napendelea kujihusisha na mijadala kuhusu maisha ya watu kabla ya kujadili undani wa imani yao. |
| 23 | Mwelekeo wangu ni kusubiri kuwaalika watu kwenye matukio maalumu ya kiinjilisti kama vile matamasha ya muziki, vyakula vya jioni,kampeni n.k. |
| 24. | Watu wanapokuwa wamefungwa kiroho, nimegundua kwamba udhihirisho wangu wa kimya wa upendo wa kikristo mara nyingine unawafanya kuwa wasikivu zaidi. |
| 25. | Motisha inayonieleza mimi ni “kufanya kitu hata kama kitapelekea hatari, lakini kufanya kitu fulani” |
| 26. | Mara nyingi ninakatishwa tamaa na watu wanotumia hoja rahisi au mantiki dhaifu. |
| 27. | Watu wanaonekana kuvutiwa wanaposikia simulizi za yale yaliyotokea katika maisha yangu. |
| 28. | Ninafurahia kuzungumza na rafiki zangu. |
| 29. | Mara nyingi ninatafuta kuhusianisha mahitaji na mivuto ya marafiki zangu na matukio mbalimbali au vitabu watakavyonufaika navyo au kuvifurahia. |
| 30. | Ninapendelea kumsaidia mtu katika Jina la Kristo kuliko kujihusisha na majadiliano ya kidini. |
| 31. | Mara nyingi naingia katika shida kwa kukosa utambuzi na busara, na kwa jinsi ninayoshirikiana/ ninavyokutana na watu wengine. |
| 32. | Ninapenda kusikia na kuelewa sababu za maoni ya watu wengine. |
| 33. | Bado ninashangazwa na jinsi Mungu alivyonivuta kumuamini yeye na ninatiwa motisha kushuhudia wengine. |
| 34. | Kwa ujumla, watu wananifikiria mimi kuwa ni mtu wa watu, mtu makini na mwenye urafiki. |
| 35. | Kitu cha kunisisimua katika juma kitakuwa kumpeleka mgeni kwenye tukio maalumu kanisani. |
| 36. | Mwelekeo wangu ni kuwa mtu wa vitendo zaidi na anayeongozwa na matendo badala ya kuwa mtu ninayeongozwa katika mawazo ya kifalsafa. |

Sasa hamisha majibu yako kwenye visanduku vyenye namba kwenye ukurasa unaofuata,na upate jumla kwa kila safu.

| WA KUKABILIANA | WA KIAKILI | WA USHUHUDA | WA KIBINAFSI | WA MWALIKO | WA KIHUDUMA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | 32 | 33 | 34 | 35 | 36 |
| JUMLA | JUMLA | JUMLA | JUMLA | JUMLA | JUMLA |
| | | | | | |

**MITINDO YA UINJILISTI**

1. **WA KUKABILIANA |** Mstari wa Wazo/Mada : 2Tim.4:2. Mfano wa Kibiblia: Petro, Matendo 2:14-23.

2. **WA KIAKILI |** Mstari wa Wazo: 2 Kor 10:5. Mfano wa Kibiblia: Paulo, Mdo 17:18,22.

3. **WA KIUSHUHUDA|** Mstari wa Wazo: 1 Yoh 1:1- 4. Mfano wa Kibiblia: mtu aliyezaliwa kipofu, Yohana 9:10,15..

4. **WA KIBINAFSI |** Mstari wa wazo: 1Kor. 9:22. Mfano wa Kibiblia: Mathayo, Lk. 5:27-29

5. **WA MWALIKO |** Mstari wa Wazo: Lk. 14:23. Mfano wa Kibiblia: Mwanamke Msamaria, Yn 4:28-30
6. **UNAOSIMAMIA HUDUMA** / **WA KIHUDUMA|** Mstari wa Wazo: Mathayo 5:16. Mfano Wa Kibiblia: Dorkasi, Mdo 9:33,36.

**KIPINDI CHA 7**

# KUPANGA KIMKAKATI

*"Lakini mambo yote na yatendeke sawasawa na kwa njia ya utaratibu." 1 Kor. 14:40*

## A. KUPANGA KIMKAKATI NI NINI?

Kupanga kimkakati kunaweza kufafanuliwa kama *"Mchakato ambao kwa huo washirika wanaoendesha shirika wanaitazamia hatima yao na kuandaa mipango na taratibu za lazima ili kufikia hatima."* Pia inaweza kuelezewa kama ni kuanza na mwisho akilini na kuchukua hatua za lazima ili kuufikia mwisho.

Baadhi ya viongozi wanaamini kupanga sio kitu cha kiroho kwa sababu wanafikiri kunawazuia kuongozwa na Roho. Wanasema kupanga kimkakati hakutoi nafasi kwa mamlaka/ enzi ya Mungu au utendaji wa Roho. Hata hivyo tunawajibika kwa Mungu kwa uwakili mzuri wa rasilimali alizotupa umiliki, na kupanga kuna nafasi muhimu sana katika uwakili huu. Sikuzote ni sharti kupanga kuambatane na maombi, tukimuomba Mungu atuongoze katika maamuzi tunayofanya.

## B. KUPANGA KUNA VIGEZO VYA KIBIBLIA

Kuna mifano ya kupanga katika Biblia. Kwa mfano, katika Mwanzo 41 Mungu alimfunulia Farao kwamba kutakuwa na miaka saba ya wingi wa chakula itakayofuatiwa na miaka saba ya njaa. Hii ilimwezesha Farao kupanga mapema ili kuokoa maisha ya watu. Katika Kutoka18; Yethro alimsaidia Musa kupangilia upya kazi ya kuwaamua watu. Musa alikuwa na lengo sahihi (kuwaongoza Israeli), lakini alikuwa anafanya kazi zote peke yake. Hili halikuwa kosa tu la kimaadili, bali alichoshwa kwa sababu alikuwa akitumia mbinu mbaya. Baba mkwe wake akampa suluhisho la nadharia ya vitendo: kuweka waamuzi juu ya maelfu, mamia, hamsini na makumi. Musa alifanya hivi, na Mungu akalibariki taifa (soma Kutoka 18).

- **Makusudi Washiriki wata…..**

  Pitia mifano ya kupanga ya kibiblia.

- Jifunze hatua za kuanzisha kanisa.

- Andaa mpango wa kufungua huduma za ibada kwa kanisa jipya.

1Goodstein,D.Leonard,Timothy M.Nolan and J.William Pfeiffer. Applied Stretegic Planning McGraw Hill,2004

Tunapendekeza kwamba washiriki wafuate hatua hizi katika makundi kwa lengo la kupanga kufungua huduma ya kanisa jipya. Baada ya kufuata mchakato, makundi washirikishe mipango yao.Kwa zoezi hili utahitaji vipande vya karatasi,tepu(gundi) na kalamu .

Kitabu cha mithali kina vifungu kadhaa vinavyorejea kupanga:

- *"... Bali fadhili na kweli zina wao wawazao(wanaopanga) mema."*( Mithali. 14:22)
- *Pasipo mashauri makusudi hubatilika, Bali kwa wingi wa washauri huthibitika.*"( Mithali 15:22)
- *Mkabidhi Bwana kazi zako, na mipango/mawazo yako yatathibitika."* (Mithali 16:3).
- *Moyo wa mtu huifikiri njia yake; bali Bwana huziongoza hatua zake."* (Mithali 16:9.)

Kitabu cha Nehemia kinatuambia jinsi Nehemia alivyopanga na kuwaongoza watu kuujenga upya ukuta wa Yerusalemu. Kwa mfano, aliyatazamia/ aliyaelewa mahitaji kabla ya kuondoka- atahitaji kitu gani kwa safari ya Yerusalemu na vifaa kwa ajili ya mji- na hivyo akaweza kupata barua kutoka kwa mfalme zinazompa ulinzi na kibali kukata miti kwenye misitu ya Mfalme (Nehemia 2:7-8).

Agano Jipya pia linazungumzia kuhusu mpango mkakati katika Luka 14:28-32, Yesu anasisitiza umuhimu wa kupanga vizuri kujenga mnara au kupanga vita. Kisha anautumia mfano huu kwa watu wanaofikiria kumfuata yeye, akiwashauri kuhesabu gharama kabla ya kuwa wanafunzi wake.

## C. KIELELEZO CHA KUPANGA (MFANO)

### 1. MCHAKATO

a. Kiongozi atawaelezea kila kundi lengo la zoezi hili. Katika kikundi chako, andaa orodha ya sehemu kuu zitakazohushwa katika kufikia lengo lako.

b. Kwa kutumia kipande cha karatasi kwa kila sehemu, andika kazi 5-10 zinazohusiana na eneo hili.

c. Bandika mawazo juu umbo au ukuta katika mtiririko wa kimantiki. Tumia kurasa mpya ili kuongeza mawazo zaidi, ukijaza kazi zinazohusiana.

d. Bainisha maeneo ya vipaumbele vya juu zaidi.

e. Yapange mawazo katika utaratibu wa matukio, ukihakikisha kwamba kila kazi ina muda unaotosha kuikamilisha.

f. Weka alama ya nyota mbele ya kazi itakayoweza kugawiwa. Andika majina ya wanaowajibika kwa kila kazi.

g. Bainisha rasilimali za ziada zitakazohitajika katika: bajeti, vifaa, raslimali,n.k.

2. **MANUFAA YA MBINU HII**.

a. Inaweza kufanyika kwa mmoja au katika vikundi.

b. Inakuruhusu kushughulikia mpango pasipo kupotea katika utondoti.

c. Inakusaidia kuainisha kile unachohitaji msaada.

d. Inakuruhusu kubadili mfululizo wa kazi kwa kugeuza tu vipande vya karatasi.

Unaweza kugeuza orodha ya kazi kuwa orodha ya kujipima ili kukusaidia kusimamia maendeleo unapotekeleza mpango.

**D. KUPANGA KANUNI KWA AJILI YA KUPANDA MAKANISA**[2]

1. **Ujuzi na maarifa.** Mtu anaweza “kujua” sana kuhusu upandaji wa makanisa, lakini kinacholeta maana ni ikiwa atauweka ujuzi wake katika vitendo. Kama ulivyo ujuzi wowote, kuanzisha kanisa kunahitaji vitendo endelevu.

2. **Anza na mwisho akilini.** Daima unapaswa kuwa na lengo la mwisho akilini unapotekeleza hatua za kuanzisha kanisa jipya. Hatua zote zinahusiana zenyewe na zimeundwa ili kuongoza kufikia kanisa jipya.

3. **Mafunzo "ya wakati tu"**. Hautahitaji kujua kila kitu unachohitaji kujua kwa habari ya kuanzisha kanisa mpaka pale utakapoanza hasa kuifanya. Kitu muhimu ni kuwa na ufahamu wa hatua za jumla katika mchakato; kisha unaweza kuamua wakati mwafaka wa kutekeleza kila hatua na namna ya kuendelea kuitenda.

4. **Tekeleza na kurudia kile kinachofaa katika muktadha**. Ukigundua kitu kinachofanikiwa vizuri, endelea kukifanya. Kwa mfano; ikiwa umepata njia iliyo bora ya kupeleka injili katika mazingira yako, hutakiwi kuendelea kuibuka na njia mpya za kuifanya.

5. **Pima maendeleo yako**. Kazi zinapaswa kupimwa kwa njia fulani ili uweze kujua kama kile unachokifanya kina ufanisi na kinazaa matunda, unaweza kupima idadi ya watu wapya unaowafikia na jinsi ulivyowafikia, idadi ya watu wanaohudhuria ibadani, n.k.

6. **"Tayari, Tekeleza, Lenga"**. Kitu cha muhimu zaidi ni kufanya kazi. Kisha unaweza kufanya marekebisho kwenye mpango wako unapoendelea. Usitumie muda wako wote kuzungumza na kupanga, pasipo kutenda.

7. **Umuhimu/Msingi wa neno.** Hatua zote unazozichukua katika kuanzisha kanisa jipya, sharti, kwa ukamilifu, ziwaongoze watu wapya kukuza uhusiano wa ndani na Mungu. Uhusiano huu unakuja kwa njia ya kusikia, kusoma, kujifunza, na kupokea neno la Mungu. (Marko 4:1-20)

Waulize washiriki kushirikisha maoni yao kwa ajili ya kufanya uhusiano na watu wapya. Mwombe kila mshiriki kuanisha ni yapi kati ya haya (maoni) ni magumu zaidi kwao na ni nani watamuuliza kwa ajili ya kupata msaada.

## E. HATUA ZA MSINGI KATIKA KUANZISHA KANISA JIPYA.

**1. Fanya mahusiano mapya**. Ziko njia nyingi zinazoweza kutumika kuwasiliana na watu wapya. Mpanda kanisa sharti ajue, kwa mfano;

- Ni wapi na kwa namna gani atawajua watu wapya.
- Namna ya kuanzisha mazungumzo.
- Namna ya kuyaelekeza mazungumzo kwenye masuala ya kiroho.
- Namna ya kumwongoza mtu mpya kwenye uhusiano na Kristo na neno lake.

Mbinu zilizo bora zaidi ni zile zinazotoa fursa ya kuendeleza mahusiano ya muda mrefu. Kila mpanda kanisa anapaswa awe wazi kujaribu njia mbalimbali za kuhubiri injili.

Baadhi ya mikakati inayowezekana ni pamoja na; Mazungumzo na watu katika jamii, Miradi ya huduma, Mikutano ya nje, Mikanda, Sherehe maalumu, Kipindi cha jioni kwa wanandoa, n.k

2. **Anzisha vikundi vidogo kwa ajili ya kujifunza Biblia**. Baada ya kufanya mahusiano mapya, mpanda kanisa anahitaji kuwajua vizuri zaidi na kuwasaidia kuuelewa ujumbe wa injili kwa undani zaidi. Vikundi vidogo vilikuwa vya muhimu sana katika kanisa la kwanza. Katika Matendo 20:20, tunaona kwamba kanisa la kwanza walikutana katika makundi makubwa hekaluni, na katika vikundi vidogo kwenye nyumba za watu mbalimbali. Kikundi kidogo ni njia bora kwa watu wapya kufundishwa. Zaidi, ni mahali salama, na panapojulikana, penye mbanano mdogo, mahali ambapo viongozi wapya wanaweza kutambuliwa na kufunzwa. Washiriki wa kikundi wanaweza kufundishwa ujuzi wa kuongoza vikundi vidogo na muda si mrefu watakuwa wakiongoza vikundi vyao wenyewe.

3. **Watie watu moyo kujitoa katika uanachama**. Hatua hii mara nyingi ni hatua inayopuuzwa sana miongoni mwa wapanda kanisa. Unawezaje kuwa na kanisa pasipo washirika? Kumbuka kwamba kujitoa kanisani ni tofauti na uamuzi wa kumpokea Kristo. Ni rahisi zaidi watu kwenda madhabahuni na kumpokea Kristo kuliko kutanganza hadharani, kujitoa sikuzote kuwa mshirika wa kanisa. Uanachama vilevile ni muhimu kwa maendeleo ya viongozi wapya. Kosa la kawaida ni kuwaweka watu kwenye nafasi za uongozi wakiwa bado hawajajitoa hadharani kujiunga na kanisa kama washirika rasmi.

4. **Anzisha ibada na kuifikia jamii**. Ibada zinaweza kuanza mara tu unapokuwa na kikundi cha msingi na mahali pa kukutana. Haijalishi ni mtindo upi wa upandaji kanisa mmeutumia, kitu muhimu zaidi ni kwamba mara tu unapoanza kuabudu, usiache. Kumbuka, uvumilivu ni alama ya mpanda kanisa. Katika ibada unatangaza hadharani kwamba mwili wa Kristo upo mahali pale. Panga ibada yako ya kwanza katika jamii kwa ujumla iwezekanavyo, na utangaze muda na mahali.

Mpanda kanisa atapaswa;

a. Kuongoza masomo katika moja ya injili na maelezo ya jumla ya Biblia, mafundisho ya msingi ya Kibiblia na mafundisho ya msingi ya kanisa. Sehemu ya ukiri/imani ya mitume inatoa mtazamo bora wa jumla wa mafundisho makuu ya mitume.

b. Waalike wanafunzi wafanye agano/kujitoa upya kwa Bwana na uwaandae kuwa washirika wa kanisa jipya.

c. Fundisha juu ya ubatizo na ufanye ubatizo.

d. Fundisha juu ya sakramenti na utoe sakramenti.

Muundo wa msingi wa Vikundi vidogo:

a. Fungua kwa swali la “kukujua wewe au kuvunja ukimya”. (Kitu ambacho si cha kibinafsi sana)

b. Ongoza somo, kwa kutumia maswali ya kutia moyo ushiriki wa kutosha.

c. Waalike watu kushirikisha mahitaji yao ya kuombea na majibu ya maombi.

d. Ombea mahitaji.

Mchakato wa kufunza Viongozi uko namna hii;

a. Ninafanya, Unaangalia.

b. Unafanya, ninakusaidia.

c. Unafanya yote, ninakusaidia kupitia jinsi ilivyofanyika.

d. Wote, mimi na wewe tunatafuta mtu mwingine ili kumfunza.

5. **Kuza uongozi.** Hatua inayofuata ni kukuza uongozi. Washirika wote wa kanisa jipya wana karama za kiroho zinazoweza kutumiwa; ufunguo ni kuzigundua karama hizi ni zipi. Uongozi unapaswa uwe matokeo ya karama zilizotolewa na Mungu kuliko uteuzi uliotolewa na mwanadamu. Njia iliyo bora ya kuwafunza viongozi ni kuwasindikiza kibinafsi na kutoa muda unaohitajika kuchangia ukuaji wao katika maeneo yote ya maisha.

6. **Kuihudumia jamii:** Kuihudumia jamii ni moja ya njia zilizo bora za kusaidia watu kujua wewe ni nani na kuona kuwa wewe ni mikono na miguu ya Yesu katika eneo hilo. Mungu anajali utu wa mtu kwa ujumla, na analiita kanisa lake kuhusika na mahitaji ya kimwili ya watu vilevile na mahitaji yao ya kiroho. (Yakobo 2:14-26). Jamii inapowaona wakristo katika matendo watu wanakuwa wazi zaidi kusikia habari za Yesu.

**POINTI ZA VITENDO:**

Amua kitakachofanyika kwa miezi mitatu ijayo:

1. Ni jinsi gani utafanya mahusiano mapya?
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

2. Unaweza kumwalika nani kushiriki kwenye vikundi vidogo, vikundi kiini, au kikundi cha kujifunza Biblia?
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

   Utafanya aina gani ya somo?
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

3. Nani yuko tayari kuja ili kujifunza kwa habari ya kuwa mshirika rasmi wa kanisa jipya?
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

   Utawaelezaje maana ya kuwa mshirika?
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

4. Utakuwa ukimfunza nani kwa ajili ya Uongozi, na utamfundishaje?
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

5. Mipango yako ni ipi kwa ajili ya ibada na huduma kwa jamii?
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

**KIPINDI CHA 8.**

# KUPANGA HUDUMA YENYE UFANISI.

*"Kila mtu kwa kadiri alivyoipokea karama,itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu".*
*1 Petro 4:10*

Kanisa lenye afya linaloongozwa na Roho Mtakatifu katika dhamira/misheni linajua namna ya kuwaunganisha waamini wapya ndani ya kanisa, kuwapokea watu wapya kwa upendo vilevile kutoa njia kwa ajili ya kuzitumia karama zao katika huduma. Kwa njia hii, waumini wapya wanakua na kujisikia hali ya umiliki na kusudi. Kipindi hiki kitakusaidia kulielewa kanisa kama mfumo na kisha kitakuwezesha kupanga mchakato kuwatoa watu kutoka mahusiano ya awali na kanisa, kuelekea ukomavu na hatimaye kuanza kujihusisha katika huduma.

Sehemu hii ni utangulizi wa awali tu, kwa kanisa kama mfumo. Mtandao wa kuzidisha unatoa taarifa zenye utendaji zaidi juu ya mada hii kwenye warsha ya kuimarisha kanisa lako.

## A. KANISA KAMA MFUMO.

Katika sayansi na dawa, watu wamegundua kwamba mwili wa mwanadamu ni kitu kimoja kilichoundwa na mifumo midogo midogo mingi; mfumo wa damu, mfumo wa neva, mfumo wa kiunzi, mfumo wa mmeng'enyo, mfumo wa hewa, n.k. Mifumo hii midogo midogo inategemeana na inahusiana-linapotokea badiliko kwa mfumo mmojawapo, mara nyingi hutokea kwa mwingine pia. Zaidi, mtu anaathiriwa pia na mazingira anayoishi. Ili kukinga, kupima, na kutibu magonjwa na kukuza usalama wa mgonjwa, daktari mzuri anaelewa umuhimu wa kujua nini kinachotokea katika mifumo mbalimbali ndani ya mtu, vilevile nini kinachotokea nje ya mazingira.

Tunaweza kulifikiria kanisa kwa njia hiyo hiyo. Kanisa ni kitu kimoja kilichoundwa na mifumo midogo midogo mingi, iliyopo katika mazingira fulani. Kujua juu ya sehemu za maisha ya kanisa na jinsi zinavyoingiliana, na kwa kuelewa muktadha ambao kanisa lipo, viongozi wanaweza kufanya maamuzi ya hekima na kusaidia kanisa kukua.

Makusudi:
Washiriki wata:

a. Elewa dhana ya mifumo na jinsi inavyohusiana na kuanzisha kanisa jipya.

b. Jifunze vidokezo/ishara tano za msingi za kanisa lenye afya.


c. Panga mchakato wa kuwatoa watu kutoka mabadiliko ya awali kuelekea ukomavu na huduma.

Kanuni muhimu za mifumo zinavyohusiana na kuanzisha Kanisa:

- Viongozi wenye afya wanaelewa kuwa kanisa ni kiumbe hai na ni shirika lenye muundo. Viongozi sharti wakumbuke kanisa zima/kamilifu wanapoendelea kushughulika na sehemu mojamoja. Kiongozi mwenye hekima huona miti pasipo kupoteza mtazamo wa msitu.

- Jukumu la viongozi ni kuhamasisha mwili unaotumika (washirika wote) kuitekeleza kazi iliyotolewa na Mungu katika muktadha wake kwa utukufu wa Mungu na upanuzi wa Ufalme wa Mungu. Viongozi wanasimamia matumizi ya rasilimali na utendaji kazi wa mifumo mbalimbali ya kanisa (huduma ya elimu, huduma za muziki wa wanawake na huduma za wanaume, n.k

Hivi ni vielelezo kumi vya msingi kwa maisha ya kanisa, ambavyo ni vya muhimu sana kwa afya ya kanisa.
Zipo sababu zingine ambazo zina athari katika ukuaji wa kanisa, kama vile muundo, mipango, Muktadha wa jamii na kanisa lilipo.




**ISHARA TANO ZA MSINGI:**

**MAONO:** Kanisa linaona kwa wa uwazi vile ambavyo Mungu analitaka liwe na lifanye kama mwili wa Kristo. Kanisa linajiingiza lenyewe kwenye makusudi ya Mungu ya ukombozi-kuleta ukamilifu katika kila eneo la maisha kupitia Yesu Kristo-kwenye jamii husika.

**TIMU YA UONGOZI:** Viongozi ndani ya kanisa wameitwa na Mungu katika nafasi zao. Ni kazi yao kuelewa maono ya kanisa, kuyaeleza maono kwa uwazi kanisani na kuupanga mwili wa Kristo ili uyafanye maono yatimie.

**UANACHAMA WA KANISA:** Washirika wa kanisa wanafanya kazi pamoja, wakitumia karama zao ipasavyo ndani ya kanisa na katika jamii, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

**RASILIMALI:** Uongozi wa kanisa binafsi na kanisa wanatengeneza mfano mzuri wa uwakili. Wanawapa changamoto washirika kuwa mawakili wazuri wa mali na vitu. Kanisa linatumia rasilimali zake za muda, vipaji na hazina ili kutekeleza kazi ya ufalme wa Mungu ndani ya kanisa lenyewe.

**ANDIKO NA MUKTADHA:** Kanisa linaelewa muktadha wake (kwa mfano, mambo ya kitamaduni, kijiografia na kijamii) na linaelewa jinsi ya kulieleza neno la Mungu kwa njia zinazoeleweka kwa wasikilizaji.

**KAZI TANO ZA MSINGI.**

**UINJILISTI:** Kanisa linatangaza habari njema za ufalme kwa neno na matendo. Kanisa linawaalika watu kuwa wanafunzi wa Yesu na kuwaelekeza kwenye uumbaji mpya.

**UANAFUNZI:** Kanisa linawasaidia watu kumuona Kristo kwa uwazi kama anavyofunuliwa kwenye maandiko, kuyajua mapenzi yake kwa ajili yao, na kumfuata katika hali zote za maisha, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

**HUDUMA:** Kanisa linahusika na mahitaji ya watu na jamii kwa Jina la Kristo katika namna kamilifu, wakiwavuta watu kuwa wanafunzi wa Kristo.

**USHIRIKA:** Washirika wanaonyeshana upendo na huruma ya Mungu, wakishirikishana furaha na mizigo. Maisha ya maombi yanaifunga jamii pamoja.

**IBADA:** Kanisa hukutana kama familia ya Mungu, na ukuu wake kwa sifa, ungamo na shukrani, wakisikiliza neno lake, na kujitoa wenyewe katika maisha ya ibada kwa utukufu wa Mungu.

Mpanda kanisa anafanya kazi pamoja na viongozi na kwa pamoja wanasimamia vidokezo hivi kumi vya maisha ya kanisa.

Sehemu hii inatupa muundo mwingine wenye mifumo midogo midogo ambayo Kanisa linaweza kuitumia kusi mamia kazi zake za msingi

**B: KANISA KAMA MFUMO:**

Katika kitabu chake cha "Makanisa Yenye Matokeo Ya Juu", Linus Morris anatoa sifa ambazo amezichunguza katika makanisa maarufu na yanayokua. Tunaweza kuziangalia sifa hizi kama mifumo midogo midogo ya kanisa.

1. **MFUMO WA MAOMBEZI:** Mfumo wa umakini zaidi ni ule wa maombi ya maombezi. Kusanyiko lina nyakati za maombi ya wote; washirika na viongozi wana utajiri wa kutosha wa maombi binafsi, kama waombezi waliowekwa kuombea huduma.

2. **MFUMO WA UINJILISTI:** Hii ni pamoja na shughuli zinazofanywa kabla ya uinjilisti, uinjilisti wa mtu kwa mtu, matukio ya kiinjilisti, na maono kwa ulimwengu.

3. **MFUMO WA MLISHANO:** Lengo la mlishano ni kuwasaidia washirika wapya kufikia uwezo wao kwa kuwahusisha wanachama kwenye huduma zifaazo kutegemeana na karama zao za kiroho.

4. **MFUMO WA LISHE YA KIROHO:** Watu wanapokea lishe ya kiroho kwa njia ya mahubiri na mafundisho ya kibiblia, vikundi vidogo na kujifunza Biblia binafsi. Imani za watu zinalishwa kupitia sakramenti: Ubatizo na meza ya Bwana.

5. **MFUMO WA KUSHEREHEKEA:** Hii inarejelea huduma ya ibada kuu au mkutano wa kanisa. Washiriki wakuu ni washirika. Mchungaji/mwalimu, kiongozi wa sifa, mkurugenzi wa mipango, wanamuziki, walimu na watu wa ufundi wanatekeleza jukumu la kuunga mkono, kusaidia kusanyiko linaposikia na kumwitikia Mungu.

6. **MFUMO WA MAFUNZO YA UONGOZI:** Timu ya uongozi inaweza kuwa na mchungaji, wazee, mashemasi na viongozi wengine. Wajibu wa mfumo wa uongozi ni kushirikisha maono kwenye mwili wote na kuhamasisha washirika kwa huduma.

7. **MFUMO WA KIUTAWALA:** Mfumo wa utawala wenye uwezo unaainisha maono, unaweka malengo, na unatengeneza mipango ili kukamilisha malengo hayo. Viongozi wanakusanya taarifa za lazima na kufikiria pointi za kuanzia, mahali ambapo kanisa linahitaji kwenda na namna ya kufika huko. Wanatumia muda wao ipasavyo, na rasilimali, na kutathimini maendeleo kuelekea kwenye lengo.

8. **MFUMO WA MAWASILIANO.** Kadri kusanyiko linavyokuwa, viongozi wanahitaji kuwasiliana kwa urasmi zaidi ili kuzuia mkanganyiko na uzembe. Timu ya mawasiliano husimamia jinsi taarifa inavyowafikia washirika (kwa mfano, kupitia matangazo, taarifa rasmi za habari, jumbe fupi za maneno, mtandao, vijitabu, barua pepe, n.k)

9. **MFUMO WA KIFEDHA:** Viongozi wanaowajibika kusimamia fedha za kanisa wanatumia utaratibu uliokubaliwa wa mahesabu. Uwazi wa suala la fedha - kushirikisha taarifa kwa uwazi kuhusiana na namna fedha ya kanisa zinavyotumika-ni muhimu kwa afya ya kanisa. Fedha zinatumika kulingana na bajeti ya kanisa, ambayo iliandaliwa na viongozi na kupitishwa na kusanyiko.

1. Orodha ya mipango yako mikuu ya huduma.
   ………………………………………… ……………………………………………….
   ………………………………………… ……………………………………………….
   ………………………………………… ……………………………………………….
   ………………………………………… ……………………………………………….
   ………………………………………… ……………………………………………….

2. Orodhesha mipango chini ya kundi linalotaka kulingana na kusudi kuu la kila mpango. Baadhi ya mipango itafaa kwenye kundi zaidi ya moja. Tazama chini kwa maelezo ya kila kundi.

| WAKUSANYE WATU | WAJENGE WATU | WAANDAE WATU | WAHAMASISHE WATU |
|---|---|---|---|
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |
| ………………………… | ………………………… | ………………………… | ……………………… |

1. **WAKUSANYE WATU:** Njia unazotumia kuwaunganisha na kusanyiko lako, kuwafanya wajisikie kukaribishwa, na kuwaalika katika uhusiano na Yesu Kristo. Mifano; Ibada maalumu, matamasha ya muziki, miradi ya huduma kwa jamii, urafiki na watu ambao si wakristo, uinjilisti wa nyumba kwa nyumba.

2. **WAJENGE WATU:** Njia unazotumia kuwafuasa watu, na kuwasaidia kukua katika imani yao. Mifano; Vikundi vya kujifunza Biblia, shule ya Jumapili, washiriki wa maombi, darasa la washirika wapya, huduma ya wanawake, huduma ya wanaume, mahusiano ya kimalezi, n.k.

3. **WAANDAE WATU:** Njia unazowasaidia watu kubainisha na kukuza karama zao na njia unazowafunza watu kwa huduma maalumu. Mifano; warsha ya uinjilisti, madarasa yanayohusu karama za kiroho, semina zinazohusiana na fedha kwa familia, kuwafunza kuongoza ibada au kuhubiri, mafunzo kwa viongozi wa vikundi vidogo, mafunzo ya gitaa, mafunzo kwa wazee/mashemasi n.k.

4. **WAHAMASISHE WATU:** Njia ambazo watu wanatumia karama zao ndani na nje ya kanisa, Mifano; Maandalizi ya chakula, kutembelea familia, kufundisha, kuongoza sifa katika ibada, kuongoza darasa juu ya shughuli fulani wanazofanya vizuri, kuwa na kambi ya mpira kwa watoto wa jirani, kusafisha kanisa, shughuli za huduma za jamii n.k Karibu kila kitu ambacho watu wanaweza kukifanya kinaweza kuunganishwa ndani ya huduma kwa kanisa.

Tunapendekeza urudie mchakato huu na viongozi kanisani kwako, na utathimini kiwango cha kujitoa kinachohitajika kwa kila mpango.

**KIPINDI CHA 9**

**KUSHINDA VIKWAZO:**

*"Duniani mnayo dhiki, lakini jipeni moyo! Mimi nimeushinda ulimwengu". Yohana 16:33*

Asilimia ya makanisa ambayo yanafunga milango yake katika miaka miwili ya kwanza iko juu. Ziko sababu nyingi za kufungwa kwa sababu ya uchanga; Kushindwa kimaadili, mikakati mibovu, na mengineyo. Hapa tutabainisha sababu mbalimbali zinazosababisha ambazo kanisa jipya linapambana nazo na jinsi ya kuziepuka.

Mara nyingi ajenda ya mpanda makanisa iko tofauti na baadhi ya washirika wa kikundi cha msingi. Kwa hali zingine, washirika wa kikundi cha msingi hawajui ajenda ya viongozi na wanaweza kukisia kwamba wana mawazo yaliyo sawa. Ajenda zinakuwa tofauti, zinajenga migogoro, matatizo, kukata tamaa, na mgawanyiko. Watu wasioshirikisha maono wanaweza kwa kupitia mitazamo yao na mawazo, kuhamisha mtazamo wao mbaya kwenda kwenye kikundi na wanaweza kuwa jiwe la kujikwaa katika kufikia misheni ya kanisa.



Tunaweza kushinda mambo magumu na migogoro tunapotafuta mapenzi ya Mungu kwa pamoja.

*"Basi ndugu, nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja".*
*1 Wakorintho 1:10*

Washiriki waangalie picha ya msichana/bibi kizee na uwaulize wanachokiona. Baadhi wataona bibi kizee tu, wengine wataona msichana tu na wengine wataona wote.
Eleza kwamba kitu kile kile kinatokea tunapokwa tunajadiliana juu ya kanisa. Iko hivi, kila mtu anaona hali kutokana na mtazamo wake, na ana mtazamo wa jinsi wengine watakavyofanya. Kwa hivyo ni jambo la uhai kuendelea kurejea maono, dhamira na maadili ya msingi ya huduma tunapofanya maamuzi na kushughulika na kutokukubaliana.

**Makusudi**.
Washiriki wata:

- Bainisha sababu zinazozuia kuanza na kukua kwa kanisa.
- Pitia namna watakavyokabiliana kibinafsi na migogoro.
- Jifunze mchakato wa kushughulika na migogoro.

Kabla hujasoma sehemu hii waombe washiriki waorodheshe mambo yanayozuia kukua kwa kanisa jipya. Yaandike haya kwenye kipande kikubwa cha karatasi na uyalinganishe na sababu zilizoainishwa hapa.

Yagawe makundi yawe mawili mawili, na uwape kazi ya kuorodhesha vizuizi katika sehemu ya A (Chomoa kizuizi kinachoonekana zaidi kwenye muktadha wako). Makundi haya yaje na majibu matatu ya jinsi/namna tunavyoweza kuviepuka vizuizi au kushughulika navyo kisha kila kikundi kutoa mawazo yao.

Hata wote wakikubaliana na maono, migogoro haiepukiki. Namna migogoro inavyoshughulikiwa itaamua ikiwa kikundi kitaendelea kusonga mbele ili kuyafikia maono.

Paulo anaposema "migawanyiko" anamaanisha "maono maradufu". Sio vibaya kuwa na maono na malengo yako, lakini ni vibaya ikiwa utalenga maono yako tu pasipo kuheshimu ama kufikiria mwili wa kanisa. Maono ya kawaida yanayoendana na Biblia, na dhamira yenye kuelekeza kwa uwazi inaweza kusaidia kuzuia kutokukubaliana kwingi ikiwa yameelezwa mara kwa mara na kama ndio msingi wa maamuzi.

## A: SABABU ZINAZOZUIA MAENDELEO YA KANISA JIPYA:

1. Kiongozi kutokuwa na karama sahihi kwa ajili ya kupanda kanisa.
2. Kukosa ukomavu kwa kikundi cha msingi.
3. Kupanga vibaya.
4. Kukosekana kwa uangalizi, msaada na uwajibikaji miongoni mwa viongozi.
5. Dhambi ndani yya uongozi.
6. Kukosekana kwa fedha.
7. Kukosa kuelewa kundi linalolengwa.
8. Matarajio yasiyo halisi.
9. Kukosekana kwa msisitizo juu ya uinjilisti na uanafunzi.
10. Kukosekana kwa muundo wa jumla kwa ajili ya kukuza huduma.

## B: MIGOGORO NDANI YA KANISA:

- Migogoro haiepukiki na ni sehemu ya kawaida ya maisha.
- Tunaweza kuchagua jinsi tutakavyoitikia migogoro.
- Maono na dhamira vinaweza kutusaidia tubaki kwenye lengo.
- Sharti tuwaruhusu watu kuondoka ikiwa hawakubaliani na maono ya dhamira ya kanisa.

  **Kumbuka:** Sio dhambi kwa kiongozi kuwa na mtazamo wa tofauti, dhambi ni kutokufaulu kushughulikia mgogoro kwa njia ya kibiblia.

## C: SABABU ZA MIGOGORO:

1. **MAKUSUDI** yasiyo wazi. Watu hawajui maono ni nini na jinsi ya kufanya ili kuyafikia. Maono, maadili na dhamira hayafafanuliwi kwa uwazi na hivyo migongano inatokea kati ya viongozi. Kila mtu ana ajenda yake binafsi, lakini uongozi wa msingi unapaswa kuwa na ajenda inayofanana.

MAKUSUDI

2. Matatizo ya **MAWASILIANO.** Kikundi cha msingi hakitoi maono na dhamira au maamuzi vizuri kanisani. Washirika hawaelezi vizuri kwa nini maamuzi fulani yanafanywa.

3. Tofauti za **KIMETHODOLOGIA**: Watu tofauti wanakabiliana na majukumu na matatizo kwa njia tofauti, mara nyingine kwa njia zisizo lingana kabisa.

4. Tofauti ya **HAIBA.** Watu wana njia tofauti za kuhusiana wao kwa wao na kuonyesha hisia (mwitikio) katika hali mbali mbali.

5. **DHAMBI:** Watu wanasema na kufanya mambo ambayo yanaweza kuumiza wengine, mara nyingine hata pasipo wao kujua.

**D. JE, BIBLIA INASEMAJE?**

Je vifingu hivi vinafundisha nini juu ya umoja na kushughulika na migogoro?.

- *"Tazama jinsi ilivyo vyema na kupendeza, watu wakae pamoja kwa umoja". Zaburi 133:1*

- *"Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi." Yohana 17:20-23*

- *"Basi ndugu, nawasihi kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja". 1 Wakorintho 1:10*

- *Na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. Waefeso 4:3*

- *"Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kifungo cha mwenzake. Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; wala msimpe ibilisi nafasi." Waefeso 4:25-27*

MAWASILIANO-KIMETHODOLOJIA-HAIBA-DHAMBI.

- *"Iweni wakarimu na wenye kuhurumiana,mkasameheane kama na Kristo alivyowasame ninyi."* Waefeso 4:32

## E. MIITIKIO MITATU KATIKA MIGOGORO:

Migogoro inaweza kuwafanya watu wasiwe na raha kabisa. Hutushtukiza na kutufanya tuseme na kutenda mambo ambayo baadaye tunajutia. Mtu anapotukwaza tunaweza kuitikia pasipo kufikiri. Mara ni kama tunateleza chini ya kilima chenye mteremko wenye kuteleza, na mambo yanahama kutoka mabaya na kuwa mabaya zaidi. Kama kielelezo katika ukurasa unaofuata kinavyoonyesha, tunaweza kusonga mbele kwa mielekeo miwili, ama kuikimbia migogoro au kuzalisha migogoro mingi zaidi. Hata hivyo kuna njia sahihi na ya kibiblia ya kushughulika na migogoro - upatanishi.

Miitikio mitatu katika migororo.


1. Kutoroka Matatizo
   - Kukataa/kukana
   - Kuepuka/Kukimbia
   - Kujiua

2. Kushambulia
   - Shambulio
   - Kushtaki
   - Kuua

3. Upatanishi (kufanya amani)

   a. Upatanisho wa kibinafsi.
      - Kuacha lipite/liende.
      - Kuzungumza.
      - Kuafikiana.

   b. Upatanisho wa kusaidiwa.
      - Upatanisho.
      - Usuluhisho.
      - Nidhamu ya Kanisa.




## F: MATOKEO YA MIITIKIO MITATU YA MIGOGORO.

| TABIA: | Kukwepa | Kufanya amani | Kupambana |
|---|---|---|---|
| MATOKEO: | "Ninapoteza" "Unashinda" | "Ninashinda" "Unashinda" | "Ninashinda" "Unapoteza" |

## G: MCHAKATO WA KUISHINDA MIGOGORO:

1. **Bainisha na ulieleze TATIZO**. Wape watu muda wa kujieleza wanafikiri tatizo ni nini na hisia zao kuhusiana na hali hiyo. Hakikisha wanazungumza na wengine na kuhusu watu wengine kwa njia ya heshima.

2. **Tengeneza SULUHISHO mbadala**. Fikirieni pamoja juu ya njia ya pili (mbadala). Jadilini faida na hasara ya kila moja.

3. **Fanya MAAMUZI**. Chagua njia iliyo bora zaidi.

4. **TEKELEZA mabadiliko**.Wawajibishe watu kwa kile wanachopaswa kufanya.

5. **TATHIMINI**. Angalia ikiwa matendo yameleta matokeo yaliyotamaniwa.

TATIZO-SULUHISHO-MAAMUZI-TEKELEZA-TATHIMINI.

**POINTI ZA VITENDO.**

1. Kwa ujumla, migogoro inapoibuka, je una mwelekeo wa kujaribu kuiepuka, kuwa mkali/mchokozi, ama kuitikia kwa njia fulani?
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………

2. Fikiri juu ya mgogoro wa hivi karibuni uliokuwa nao na mtu fulani (au mfano wa hivi karibuni ambapo mtu fulani alikuchanganya). Je, ugomvi ulihusu nini? Je,ulikabilianaa nao kwa vipi?(Kwa Kutoroka? Kwa kushambulia? Kwa jaribio la kufanya amani?) Je kitu gani ungefanya tofauti kwa wakati ujao?
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………..
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………

3. Washiriki wa kikundi washirikishe baadhi ya mifano ya migogoro ambayo inaibuka kanisani. Shughulika na mgogoro kwa kutumia hatua zilizopo sehemu G, "Mchakato wa Kuishinda Migogoro"
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………..
   …………………………………………………………………………………………………

**KIPINDI CHA 10**

# KUIANGALIA FAMILIA YAKO NA KUJIANGALIA WEWE MWENYEWE.

*"Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa", Wakolosai 3:21*

Familia ya mpanda kanisa sharti iwe KIPAUMBELE. Ikiwa umeoa/umeolewa unapaswa kuweka kiwango cha juu cha umuhimu wa kutunza mke na watoto wako. Kwa bahati mbaya, wapanda makanisa wengi wanapatikana masaa 24 kwa siku ili kukutana na mahitaji ya huduma zao, na ya watu wengine, na wamekuwa wageni kwa familia zao. Hata kama hujaoa/hujaolewa bado unapaswa kuweka mpaka ili uweze kujijali wewe mwenyewe, uwe na mahusiano mazuri na usije ukachoka sana.

## A: MANUFAA KWA MPANDA KANISA NA FAMILIA YAKE:

Upandaji wa kanisa hutoa fursa ya;

- Kukutana na mahitaji ya msingi zaidi ya kisaikolojia ya watu wengine-kuwapenda na kupendwa, na kujisikia wa maana kibinafsi na kwa wengine.
- Kukua na kuendelea kama kiongozi.
- Kuwatumikia watu katika matukio ya muhimu zaidi ya maisha ya ndoa, kuzaliwa, mazishi n.k
- Kumwona Mungu akitenda kazi katika maisha ya watu na kuona watu waliopotea kiroho wakiyageuza maisha yao kwa Kristo.
- Kukuza karama zako za kiroho na kuisaidia familia yako kukuza karama zao.
- Kuonyesha kielelezo cha nini maana ya kuwa mtumishi wa Kristo kwa watoto na ndugu.
- Kuvuka mpaka wako wa starehe na kuwafikia watu wengine kwa injili.

Kabla hujawasilisha sehemu hii, waombe washiriki kutoa maoni yao juu ya namna mpanda kanisa na family yake watabarikiwa kwa kuanzisha kanisa.

Baada ya kuwasilisha sehemu hii, waombe washiriki kufikiria mfano wa binafsi wa manufaa yaliyoorodheshwa.Waombe wayashirikishe katika makundi matatu au manne. Kumbuka kwamba si washiriki wote wote wameoa/kuolewa-Mungu anawaita wengi kumtumikia wakiwa peke yao (1Kor 7:1,7-8,17), wazazi, ndugu na marafiki wana nafasi muhimu katika kulea na kumtumia mpanda kanisa.

Makusudi:
Washiriki wata:……..

- Jadili manufaa na hatari kwa familia ya mpanda kanisa.
- Panga namna watakavyojifunza wao na familia zao.

## B. HATARI KWA FAMILIA ZA MPANDA KANISA;

Waulize washiriki kama wamemwona mchungaji moja kwa moja na nini kinachoweza kutokea pale mchungaji anapopuuza familia yake.

- Kukosa mipaka. Kama zimeruhusiwa, huduma na mahitaji yake yatakula muda wako na nguvu.
- Kujaribu kukutana na matarajio yasiyo halisi, aidha yako mwenyewe au ya wengine.
- Kubadilishana uhusiano wa ndani na mwenzi wako, familia au marafiki kwa kazi ya huduma.
- Kujitenga katika mazingira mapya na yasiyofahamika, mbali na msaada wa familia na marafiki.
- Kutojali fursa za familia kukua pamoja.
- Kupalilia hali ya kutegemeana kwa kujihusisha kihisia na watu wenye mahitaji mengi.
- Nyumba zimeshindwa kuwa kimbilio salama ambapo kila mwanafamilia (na wewe ukiwemo) anapata mahali salama pa kuwepo na kueleza mawazo yao na hisia zao.

Baada ya kusoma sehemu hii, washiriki wajibu maswali yaliyo chini ya sehemu ya kumi ya pointi za vitendo namba 1. Wanapomaliza kujibu waombe kubainisha kile wanachojifunza juu yao wenyewe.

Sehemu C na D zimekusudiwa kuwa fupi ili muda mwingi utolewe kwa washiriki kwa ajili ya mapitio binafsi katika sehemu/kipengele cha pointi za vitendo.

## C: KUJIJALI WEWE MWENYEWE.

Yesu alipoulizwa amri iliyo kuu ni ipi, alisema amri ya kwanza ni kumpenda Mungu na pili ni kumpenda jirani kama nafsi yako. (Marko 12:30-31). Hakusema, kutojipenda nafsi yake, zaidi alijua kujipenda mwenyewe ilikuwa sehemu ya kawaida ya kuwa mwanadamu. Watu wanaposafiri kwenye ndege, maelekezo ya usalama yanasema kwamba, ikiwa vifaa vya oksijeni vitahitajika, vaa kifaa chako kwanza kisha wavalishe watu wanaosafiri pamoja nawe. Hii ni kwa sababu kama hautapata hewa ya oksijeni, hautaweza kumsaidia jirani yako. Kanuni ile ile inafaa katika huduma ya kupanda kanisa. Wapanda kanisa lazima wajijali wao wenyewe ili kuweza kuyashughulikia mahitaji ya huduma.

**D. KUINGALIA FAMILIA YAKO**

Tukiwaambia wenzi wetu na watoto wetu ya kwamba Mungu anawapenda, lakini hatuwaoneshi upendo wa Mungu - kwa kutumia muda pamoja nao, kuwasikiliza, kucheka nao, kulia pamoja nao, kuwahudumia, na kuwashirikisha uzima-hawatatuamini. Paulo anawaita wanaume kuwapenda wake zao kama Kristo anavyolipenda kanisa (Waefeso 5:25). Kitabu cha Kumbukumbu kinawaita wazazi kuwafundisha watoto juu ya Mungu, "ukaapo nyumbani,utembeapo njiani,ulalapo na uamkapo"(Kumb 6:7).

Baada ya kusoma sehemu hii, washiriki wajibu maswali ya marejeo yaliyopo sehemu ya 10 ya pointi za vitendo ili kubainisha mahusiano na wenzi wao na familia (au na familia zao na marafiki ikiwa hawajaoa/hawajaolewa)

Haya yote yanahitaji uwepo wa kimwili na kihisia. Kuwa hapa kihisia kunamaanisha kuendana na yale ambayo wengine wanafikiri na kujisikia na kupata muda wa kuuliza jinsi walivyo na wanavyosikia hasa yale wanayoyasema.

Kumbuka, muda ukiruhusu na ukiongozwa na kiongozi wa warsha, soma kiambatanisho cha 1 sehemu C: Familia.

# POINTI ZA VITENDO.

I. Kujijali mwenyewe: Jitathimini wewe mwenyewe kwa maeneo yafuatayo:-
(1= Sivyo ilivyo na 5= Sawa Kabisa)

1. Maisha na Mungu:
   a. Ninatumia muda kila siku kusoma neno la Mungu na kuomba.
      1 2 3 4 5
   b. Nina mtu ambaye ninawajibika kwake na anayenipa ushauri wa kiroho.
      1 2 3 4 5

2. Usalama wa kimwili.
   a. Ninafanya mazoezi, ninakula vizuri, na kupata mapumziko ya kutosha.
      1 2 3 4 5
   b. Ninapokuwa mgonjwa ninapumzika au kupata uangalizi wa kitabibu.
      1 2 3 4 5

3. Usalama wa kihisia.
   a. Ninapopata hasira, ninatumia njia chanya kukabiliana na kushughulikia hali hiyo.
      1 2 3 4 5
   b. Ninapokuwa na huzuni; neno la Mungu, wapendwa na marafiki, kupumzika, na ibada vinanirejeshea hali ya furaha.
      1 2 3 4 5

4. Mahusiano:
   a. Ninatumia muda na nina mahusiano na familia na marafiki.
      1 2 3 4 5
   b. Mwenzi wangu na mimi (au marafiki na mimi) wanashiriki furaha yetu na matatizo yetu na wanajua kila mmoja ni wa muhimu kwa mwingine.
      1 2 3 4 5

5. Fedha:
   Familia yangu na mimi tunasimamia fedha zetu vizuri ili tuwe na kiasi cha kutosha kutusaidia kuishi.
   1 2 3 4 5

6. Ukuaji:
   Mwaka uliopita nilipata fursa kujifunza kitu kipya.
   1 2 3 4 5

**II. Kuingalia Familia: Kama uko peke yako, jibu maswali haya kwa namna ya familia na marafiki wa karibu.**

1. Ni muda gani umepita tangu ulipozungumza na kumuombea mwenzi wako?
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

2. Je, unatumia muda upi katika juma kuwa pamoja na familia nzima na kila mshirika kibinafsi?
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

3. Je, hofu za mwenzi wako/familia yako juu ya upandaji wa makanisa ni zipi?
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

4. Je hofu zako binafsi juu ya upandaji kanisa ni zipi?
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

5. Je, ni sehemu zipi za huduma mwenzi wako/familia yako wana mzigo/shauku nazo?
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

6. Je, mwenzi/wanafamilia wana karama zipi?
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

7. Je, ni kwa vipi utu wa mtu, karama na mivuto ya mwenzi/wanafamilia inaamua ushiriki wake katika huduma?
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

8. Je ni mambo yapi mengine (familia, taaluma ama vyovyote vile) ambayo mwenzi/familia wanajitoa kwayo?
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

9. Je, utamlindaje mwenzi wako/familia kutokana na matarajio yasiyo yakini?
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

10. Je umejadili na kufikia makubaliano na familia yako juu ya;

- Simu zinazopigwa nyumbani (miito ya simu nyumbani)
- Siku za mapumziko.
- Masaa ya usiku.
- Shughuli za kiofisi nyumbani.
- Mambo yanayohusiana na kanisa kufanyika nyumbani mwako.

III. Kwa kutegemea majibu ya maswali yaliyopo juu, andika ni mambo gani mawili unahitaji kuyafanya.

1. Kujiangalia wewe mwenyewe kwa uzuri zaidi;
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

2. Kuimarisha uhusiano na familia yako.
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

Kiambatisho cha 1 |

# MAFAFANUZI

## A. MAOMBI

“Leo tunatamani sana maombi, na tunajificha na maombi. Tunavutiwa na maombi na tunasukumwa nayo. Tunaamini maombi ni kitu tunachopaswa kukifanya, hata kitu tunachotaka kukifanya, lakini inaonekana kama shimo kubwa limesimama kati yetu na kuomba hasa (kwa vitendo).Tuna mzigo wa kutokuomba.

Hatujui hasa ni nini kinachotuzuia. Ukweli, tuna kazi nyingi na majukumu ya kifamilia, lakini hivyo ni kuficha tu ukweli.(…) Hapana, kuna kitu cha undani zaidi, kitu kizito zaidi kinachotuzuia kujichunguza. Kwa ukweli, kuna idadi ya “mambo yanayotuzuia ambayo tutayachunguza kwa wakati mwafaka. Bali kwa sasa kuna “jambo” moja linalihitaji kuliangalia zaidi kwa haraka. Ni fikra… kwamba lazima kila kitu “kiwe sawa” ili tuweze kuomba. Ni kwamba, kabla hatujaomba hasa, maisha yetu lazima yawe na utaratibu/mwelekeo mzuri, au tunahitaji kujua zaidi juu ya jinsi ya kuomba, au tunahitaji kujifunza maswali ya kifalsafa yanayohusiana na maombi, au tunahitaji kuyashika vizuri zaidi mapokeo makuu ya maombi. Na kuendelea. Hayo si mambo yasiyo sahihi au kwamba hakuna muda kabisa wa kushughulika nayo. Lakini tunaanza na mwisho wa maombi usio sahihi - tunaweka mkokoteni mbele ya farasi. Tatizo letu ni kwamba, tunadhani maombi ni kitu fulani kinachohitaji uzoefu/utalaamu kama tunavyozoea aljebra au ufundi magari. Hii inatuweka kwenye nafasi ya juu “mahali” ambapo tuna uwezo na umiliki. Lakini tunapoomba, tunashuka “chini”, mahali ambapo kwa utulivu na kunyenyekea zaidi hutawala na kutufanya kutokuwa na uwezo. (…)

Ukweli wa jambo ni huu, sote tunakuja kwenye maombi pamoja na lundo la msongamano wa uungwana na ubinafsi, wenye rehema na chuki, wenye upendo na uchungu. Kweli, upande wa umilele kamwe hatutafumbua mema kutoka mabaya, yaliyo safi kwa yasiyo safi. Lakini nilichokiona ni kwamba Mungu ni mkuu wa kutosha kutupokea na mchanganyiko wetu. Hatuhitaji kuwa wasafi sana au waliojaa imani ama chochote kile. Hivyo ndivyo neema inavyomaanisha, na siyo kwamba tumeokolewa kwa neema tu, bali tunaishi kwa neema pia. Na tunaomba kwa neema.

## B. NENO LA MUNGU

Sehemu kubwa ya Theolojia yetu (…) inategemea uzoefu, lakini kama wakristo, hiyo siyo nguzo pekee; maisha ni lazima yaeleweke kwa nuru ya maandiko. Kujikosoa ambako kanisa linaweza kufanya kunalenga juu ya maandiko na tafsiri yake sahihi, kuanzia ukweli mmoja: tunapaswa kusoma Biblia zaidi. Tunasikiliza jumbe nyingi kila Jumapili na katika juma kwenye radio na televisheni, vile vile tunasoma majarida na vitabu, lakini tunasoma Biblia dakika chache tu kwa siku, labda kwa kuhusiana na mradi maalumu wa usomaji Biblia kwa mwaka mmoja. Na kama tukisoma Biblia zaidi tunasoma tafsiri/Toleo moja tu la maandiko, tukikosa uwezekano wa kutajirisha ufahamu wetu wa Neno la Mungu kwa tofauti ndogo au tafsiri tofauti za lugha za asili.

1. Foster, Richard J. Prayer: Finding the Hearts True Home Happen Collins, 1992, pp 7-8

Mashaka mengi, upotofu na sintofahamu nyingi tulizo nazo juu ya maandiko zinaweza kuwekwa wazi na maandiko yenyewe; tunahitaji kutenga muda kila siku kusoma, kuzama, kwa umakini, tukisoma ili kuelewa mandhari pana zaidi ya andiko, tusome kwa hali ya ibada na upendo. Kwa hatua ya baadaye, tunahitaji kujifunza Biblia na kutafakari ili kuongeza ufahamu wetu wa Neno la Mungu.

Kujifunza Biblia: Kusudi lake ni kuchunguza au kushika maana za ndani za andiko la kibiblia. Inaainishwa kwa kuchambua sehemu ndogo zaidi ya andiko la kibiblia. Kujifunza kunahusisha uchunguzi makini wa jinsi sehemu tofauti za kifungu zinavyohusiana.

Tafakari za kibiblia: Kusudi lake ni mazungumzo ya ukaribu na Mungu. Inabainishwa na kufikiri polepole juu ya mstari wa kifungu cha andiko. Inasisitiza uhusiano wa karibu zaidi na Mungu na jibu binafsi kwa Neno lake.

“Ni vizuri kujua kwamba mitazamo hii mitatu ya Biblia (kusoma, kujifunza na kutafakari havitenganishwi. Kila kimoja kina thamani na matumizi yake, kutegemeana na kundi la msomaji. Ni muhimu pia kukumbuka kwamba kila njia tunapoikaribia Biblia ni jibu la Mungu mwenye kuanzisha. Katika Ebr. 1:1 tunasoma kwamba Mungu alitumia njia nyingi kuwasiliana nasi. Waraka huo huo unatuambia katika sura ya 4:12, kwamba Neno lake li hai, tena lina nguvu na huzama katika vilindi vya utu wetu, ili kutimiza makusudi ya Mungu ya milele.

## C. FAMILIA

Watoto wote wanahitaji kupendwa na wazazi na wao wenyewe kupenda wazazi wao. Mahitaji matano yaliyoorodheshwa hapa chini kwa watoto ili wawe na uhusiano unaofaa na wazazi wao. Wakati baadhi ya vidokezo vinapokosekana katika uhusiano wa kifamilia, uwezo wa kupokea na kutoa upendo unaathiriwa au unakuwa na mipaka.

- Usalama – kujisikia salama nyumbani
- Kuwa mali ya – kujisikia kwamba wewe ni sehemu ya familia ni familia ya na wanakukubali na kukuthamini.
- Mipaka – kuwa chini ya nidhamu yenye upendo na iliyo thabiti.
- Jamii – kuwa sehemu iliyo hai ya jamii au ujirani
- Mnyumbuliko – fursa za kushiriki, na kutoa maoni ni hisia.

**Mambo yanayoharibu mawasiliano katika ndoa.**

Kulingana na kitabu cha *"Kupigania Ndoa Yako",* yafuatazo ni baadhi ya mambo yanayoharibu mawasiliano na ambayo yanaweza kukuza ugumu katika ndoa.

- Ukali: Pale mazungumzo yanapoanza kupanda ngazi kuelekea hisia mbaya badala ya kujibu kwa sauti nyororo na kujaribu kuelewana hisia za kila mmoja kwa unyofu.

- Kupuuza/Upuuziaji: Namna ambayo mtu mmoja hupuuza mawazo, hisia au tabia za mwenzi. Upuuziaji hujenga mipaka katika uhusiano ambao hauhesabu mtazamo wa mwenzi.

- Tatsiri zisizo sahihi: Hii hutokea pale mwenzi anapotafsiri kila mazungumzo au matukio kwa njia mbaya na nafasi yoyote ya kitu kilicho chema. Tafsiri hizi zina kawaida ya kuhoji ama kuonea shaka nia za mwenzi.

- Kujiondoa na kukwepa: Mara nyingi mwenzi anafuatilia masomo fulani au majadiliano na mengine anayaepuka. Ni vigumu kusuluhisha mgogoro vyema ikiwa wanandoa hawatii juhudi yoyote makini kushughulikia migogoro.

**Sababu za kawaida na kubwa zinazoongezwa matengano kwa wanandoa**

**Zisizo za Moja kwa moja( za kawaida):**
- Utu wa mtu unaoitikia matatizo kwa nguvu
- Kuwa na wazazi waliopitia talaka
- Mahusiano ya kimapenzi kabla ya ndoa
- Kuwa mtu uliyepitia talaka
- Kuwa na watoto kutoka kwenye ndoa nyingine
- Kuwa na asili tofauti na taratibu tofauti za kidini
- Ndoa katika umri mdogo sana
- Kutokufahamiana vizuri kabla ya ndoa
- Matatizo mazito ya kiuchumi

**Sababu zenye nguvu (Za moja kwa moja):**

- Mitindo hasi ya mazungumzo na mapambano
- Ugumu katika kuwasiliana kwa namna yenye afya
- Ugumu katika kukabiliana na migogoro
- Matarajio yasiyo halisi katika ndoa
- Kujitoa kwa kiwango cha chini kati ya wana ndoa
- Kutokufanyia kazi maisha ya imani kwa pamoja

7. Markman, Stanley and Blumberg. *Fighting For You Marriage*

## C. UINJILISTI

**Mkakati wa Uinjilisti na ufuatiliaji makini wa waamini wapya**.

Iko mitindo mingi ya uinjilisti ambayo imethibitisha ubora wake.Mmojawapo ni mradi wa Philipo. Ni mkakati rahisi sana ambao umesaidia maelfu ya makanisa duniani kote. Unahusiana na kumpatia mtu nakala ya Injili ya Yohana, na Mwongozo wa kujifunzia unaodumu kwa majuma matano. Unapokutana na mtu, unakuza uhusiano naye mnapoendelea kujifunza Neno pamoja, kupeleka Injili, na kuomba pamoja. Baada ya mafunzo ya awali, watu wanaalikwa kushiriki katika kikundi cha kujifunza Biblia. Watu wengi wanajiunga na kanisa kwa njia hii. Mradi wa Filipo pia unatoa vifaa vya ufuatiliaji na uanafunzi vyenye msingi juu ya maandiko na vinatoa mafunzo ya muhimu kwa kanisa lako.

Hapa tunatoa mfano uliofupishwa

**Mradi wa Filipo nini?** Ni mkakati wa Uinjilisti na uanafunzi kaw kanisa la mahali pamoja. Misingi ya kibiblia kwa mkakati huu ni Mdo. 8:26-40. Hadithi ya Filipo kukutana na Towashi wa Kushi (Ethiopia) inatufundisha kanuni tatu kwa habari ya kuwafikia watu kwa ajili ya Kristo:

1. **Uinjilisti:** Kuliweka Neno la Mungu kwenye mikono ya watu. Mkushi anasoma Neno la Mungu katika kitabu cha Isaya na anahisi kwamba anahitaji kujua zaidi.
2. **Uanafunzi:** Kufuatilia waamini wapya. Filipo akiongozwa na Roho, anakielezea kifungu cha Isaya na anampa habari njema.
3. **Uanachama:** Kumwongoza mtu katika kujitolea kanisani, Mkushi, baada ya kumsikiliza Filipo anauliza ikiwa anaweza kubatizwa na kwa njia hii anajiungamanisha na mwili wa Kristo.

**Somo la Yohana**
Akina “Filipo” waliofunzwa kimkakati wanaliweka Neno la Mungu katika mikono ya watu wanaokusudia kukutana nao tena. Lengo ni watu wamjue Mungu na kujitoa ndani ya kanisa. Kuna mfano wa somo la kwanza wa kujifunza Biblia kwa jumla uliotumiwa na wanaopokea mwaliko kujifunza moja ya Injili.

- Dakika 5 – kamilisha maswali yafuatayo kwa kutumia Injili ya Yohana tu, kulingana na rejea za kibiblia baada ya kila swali.
- Dakika 15 – baada ya kujibu maswali, kutana na watu wawili au watatu ili kushirikisha majibu yenu. Kila mtu aongoze kikundi kwa zamu.

**Juma la kwanza – Somo la kwanza (sura ya 1-5)**

1. Ni nani aliyeumba uzima na ni nuru ya watu? (1:4)
2. Tunapaswa kufanya nini ili tuwe na haki ya kufanyika watoto wa Mungu? (1:12)
3. Je, tunamjua Mungu, pendo lake, na kweli yake kupitia kwa nani? (1:17,18).
4. Je, Yesu, mwanakondoo wa Mungu, anafanya nini kwa ajili ya ulimwengu na pia kwa ajili yako? (1:29)
5. Je, Yesu alionyesha nini kupitia muujiza wake wa kwanza? (2:11)
6. Je, nifanye nini ili niwe katika ufalme wa Mungu? (3:3)
7. Kwa nini Mungu alimtoa mwanawe pekee ili kutuokoa sisi? (3:16-18)
8. Je, wale waliomwamini wana nini? Nini kitatokea ukimkataa? (3:36)
9. Je, wasamaria walijua nini kwa habari za Yesu baada ya kutumia muda na Yeye? (4:40-42)
10. Nini kinatokea ukiyasikia maneno ya Yesu na kuyaamini? (5:24)

**Kumbuka**| Kanisa lako linaweza kuunda masawali yake lenyewe kwa kutumia moja ya injili. Maelfu wanamjia Kristo kwa njia hii.

Kiambatisho cha II|

# MITINDO SITA YA UINJILISTI

1. **WA KUKABILIANA**
   **Mstari wa Mada/Somo**: 2Tim. 4:2, Mfano wa Kibiblia: Petro, Mdo. 2:14-20.
   **Mifano ya Sasa**: Billy Graham, Luis Palau.
   **Tabia:** Una ujasiri binafsi, kuthubutu, ujasiri, mkweli na mtiifu.
   Mara nyingi unaelekea kwenye pointi katika mazungumzo.
   Una maoni na usadikisho wenye nguvu sana.
   **Tahadhari:** Tafuta hekima ya Mungu ili kuwa makini na mwenye tahadhari. Mruhusu Roho Mtakatifu kulainisha uelekeo wako ili kutia mkazo imani yako inapokuwa ni lazima. Jiepushe na kuhukumu wale wanaotumia aina nyingine ya mitindo ya Uinjilisti.

2. **WA AKILI**
   **Mstari wa Mada**: 2Kor. 10:5. Mfano wa Kibiblia: Paulo, Mdo. 17:18,22.
   **Mifano ya sasa**: Josh McDowell.
   **Tabia:** Unapenda kupambanua/kuchambua mambo, una mantiki sana, wenye uchunguzi, na wenye udadisi. Unapenda kuhojiana.
   **Tahadhari**: Epuka kupotea katika mahojiano ya kitaaluma. Kumbuka kwamba mtazamo wako ni wa muhimu kama ilivyo taarifa. 1Petro 3:16 unasema kwamba tunapaswa kujibu kwa upole na heshima.
   Epuka kuwa mbishanaji au kufungua ubishanaji.

3. **WA USHUHUDA**
   **Mstari wa Mada**: 1Yn. 1:1-4. Mfano wa Kibiblia: Mtu aliyezaliwa kipofu, Yn. 9:10-15.
   **Mifano ya sasa**: Nicky Garza, Corrie Ten Boom, Joni Erickson.
   **Tabia:** Ni mwasilianaji mzuri na msemaji mzuri. Uko wazi juu ya maisha yako binafsi, hofu zako na mafanikio yako.Unastaajabu kwa yale ambayo Mungu ameyafanya katika maisha yako. Unaona uhusiano kati ya uzoefu wako na wa watu wengine.
   **Tahadhari**: Hakikisha unahusianisha uzoefu wako kwa maisha ya wasikilizaji. Hii inakudai kusikiliza sana kwanza ili kujua vya kutosha juu ya maisha ya watu wengine ili kulinganisha/kufanya muunganiko. Usiushushe uthamani wa uzoefu wako kama unahisi ni wa kawaida sana, hadithi za kawaida ndizo ambazo “watu wa kawaida” hupenda kuiga.

4. **WA KIBINAFSI**
   **Mstari wa Mada**: 1Kor. 9:22. Mfano wa Kibiblia: Mt., Lk. 5:27-29.
   **Mifano ya sasa**: Joe Aldrich (mwandishi wa kitabu cha *Uinjilisti wa Mtindo wa Maisha*.
   **Tabia**: Unapenda kuzungumza, na una huruma na makini. Unatafuta urafiki na unalenga juu ya watu na mahitaji yao.
   **Tahadhari:** Usithamini urafiki zaidi ya ukweli. Unahitaji kuwaonya marafiki zako kwamba ni wenye dhambi na wanahitaji mwokozi. Usihofu kupitiliza juu ya mahitaji ya marafiki zako; saidia kadiri uwezavyo, na yaliyobaki umwachie Bwana.

5. **WA MWALIKO**

**Mstari wa Mada**: Lk. 14:23, Mfano wa Kibiblia: Mwanamke kisimani, Yn. 4:28-30
**Mifano ya sasa**: Ruth Graham
**Tabia:** Ni mkarimu, na mwenye ushawishi, unafurahia kukutana na watu wapya. Unaona matukio ya Uinjilisti kama fursa ya kipekee.
**Tahadhari:** Uwe makini kutokuwaachia mara kwa mara watu wengine waseme kwa niaba yako. Rafiki zako na jamaa zako wanahitaji kujua vile Kristo alivyokubadilisha. Aidha, rafiki zako wana maswali ambayo ungeyajibu juu ya maana ya Injili katika maisha yao. Fikiri kwa umakini na kwa maombi juu ya matukio au huduma ambazo utawaalika watu. Usisikitishwe ikiwa hatakujali, kukataa kwao kunaweza kuwa fursa ya mazungumzo ya kiroho. Pia “hapana” yao ya leo yaweza kuwa “ndiyo” kesho.

6. **WA KUTEGEMEA IBADA**

**Mstari wa Mada:** Mt. 5:16, Mfano wa Kibiblia: Dorkasi, Mdo. 9:33,36
**Mifano ya sasa**: Mama Theresa
**Tabia:** Unavumilia. Unalenga sana juu ya watu wengine. Unaona mahitaji na unafurahia kushughulika nayo.
Unaonyesha upendo wako kupitia matendo yako zaidi ya maneno. Unashughulika na majukumu ya kiunyenyekevu kwa bidii.
**Tahadhari**: Kumbuka kwamba kama yalivyo maneno mazuri pasipo matendo mazuri yanatuchanganya, ndivyo yalivyo, matendo mazuri pasipo maelezo/mafafanuzi. Rum. 10:14, inatuambia kwamba tunapaswa kueleza habari za Kristo ili kwamba wengine wasikie. Usiishushe thamani ya ibada yako (matendo yako). Mtindo wako utawafikia wale walio mbali na Mungu au wenye hasira na Mungu.
Matendo ya huduma ya upendo ni vigumu kuyakataa au kupingana nayo.

Kiambatisho cha III

# UKARIMU

## Kulifanya kanisa lako kuwa lenye ukaribisho zaidi

*"Nyingi kati ya njia za mawasiliano ambazo ulimwengu unazitumia si dhambi, na zingepaswa kutumiwa na kanisa. Msalaba wa Kristo ni kikwazo kidogo zaidi kwa wasioamini kuliko mbinu/taratibu zinazotumiwa na baadhi ya wakristo kuwasilisha Injili"* (Knute Larson)

*"Tusiwe kwazo la namna yoyote katika jambo lolote,ili utumishi wetu usilaumiwe; bali katika kila neno tujipatie sifa njema,kama watumishi wa Mungu"* (2Kor. 6:3,4)

*"Asilimia sabini ya wale wanaotembelea makanisa yetu wanafanya uamuzi wa kurudi tena ama kutokurudi tena KABLA Mchungaji hajasimama kuhubiri"* (Barna Research Group) (Kikundi cha Utafiti cha Barna).

Chini utapata orodha ya vidokezo vya kufikiria kwa ibada ya Jumapili na kwa kanisa kwa ujumla. Unaweza kuhusisha /kuweka vidokezo vingine. Unapofanya zoezi hili, jaribu kujiweka mwenyewe mahali pa mshirika mpya na uangalie mambo kama ndio ulikuwa unayaona kwa mara ya kwanza.

**1. Ishara**
- Ishara zinazoonesha vyoo, chumba cha watoto, au maegesho ya magari yalipo.
- Herufi kubwa zinazoonekana.
- Kauli mbiu iliyopo (ya sasa).
- ______________________________
- ______________________________

**2. Ibada**
- Safi na zenye Ukaribisho.
- Usafi wa vyoo na kupewa vitu vyote muhimu mapema/kabla, wakati wa ibada na baada ya ibada.
- Ni rahisi kupata mahali pa maegesho na ni pa kutosha.
- Maeneo yanaendelezwa/yanatunzwa vizuri.
- ______________________________
- ______________________________

**3. Wahudumu na Ukaribisho.**
- Wenye urafiki na wenye taarifa sahihi/nzuri.
- Uwiano kati ya jinsia.
- Uwakilishi wa rika mbalimbali.
- ______________________________
- ______________________________

4. **Malezi ya watoto.**
    - Mfumo ulio salama.
    - Watenda kazi waliofunzwa.
    - Makabrasha yanayoelezea mfumo.
    - ________________________________
    - ________________________________

5. **Hali ya hewa/Mazingira**
    - Kuna muziki wa asili
    - Mwanga mzuri
    - Mapambo
    - Sehemu nzuri za kukaa, rahisi kufikika
    - ________________________________
    - ________________________________

6. **Wakurugenzi wa Ibada: Viongozi wa Sifa, Mchungaji nk.**
    - Wema na wenye shauku
    - Ni thabiti
    - Wanavaa kwa unadhifu
    - ______________________________
    - ______________________________

7. **Lugha**
    - Iko wazi (uwe makini na “lugha za kanisa”)
    - Ni ya wote/inahusisha wote
    - ____________________________
    - ____________________________

8. **Muziki na Uimbaji**
    - Ubora kimuziki
    - Theolojia ya muziki imethibitishwa/imehakikishwa
    - Maneno ya wimbo yanayoeleweka na yanayoonekana.
    - ____________________________
    - ____________________________

9. **Utaratibu wa Huduma ya Kuabudu**
    - Imepangiliwa
    - Inaanza kwa wakati na inatiririka vizuri
    - Ina vitu mbalimbali (maigizo, video nk)
    - ______________________________
    - ______________________________

10. **Masomo yaliyochapishwa**
    - Yameandikwa vizuri (ni safi, rahisi kuyasoma)
    - Hayana makosa ya kiuandishi/tahajia
    - ___________________________
    - ___________________________

# TAARIFA FUPI YA MPANDA KANISA

## TAARIFA ZA BINAFSI

PICHA

JINA LA UKOO:

JINA LAKO:

CHEO: UMEOA/UMEOLEWA:

JINSIA: TAREHE YA KUZALIWA: UMRI: IDADI YA WATOTO:

ANWANI: NAMBA YA SIMU:

JIJI: JIMBO: NCHI: BARUA PEPE:

## TAARIFA YA ENEO AMBAKO KANISA JIPYA LITAPANDWA

JINA LA KANISA: ANWANI:

JIJI: JIMBO: NCHI:

## TAARIFA ZA KANISA MAMA

JINA LA KANISA: JINA LA MCHUNGAJI:

ANWANI: UJIRANI / KIJIJI:

JIJI: JIMBO: NCHI:

**USHUHUDA WA MPANDA KANISA**

**INAENDELEA UPANDE UNAOFUATA**

**MAHITAJI YA KUOMBEA**

1. ______________________________________________
______________________________________________
2. ______________________________________________
______________________________________________
3. ______________________________________________
______________________________________________

________________________
Sahihi ya Mpanda Kanisa

_______/ ____/ _____
Mwezi/Siku/Mwaka

# ABC ZA MPANDA KANISA

**TAARIFA YA KILA MWEZI**

## TAARIFA YA JUMLA

| | |
|---|---|
| **MWEZI WA RIPOTI** | |
| **JINA LA MPANDAKANISA** | |
| **KANDA ANAYOTOKEA** | |
| **MRATIBU WA KANDA** | |

## TAARIFA ZA BINAFSI

| | |
|---|---|
| **WATU WAPYA ULIOWAFIKIA**<br>WATU ULIOWAFIKIA KATIKA MAZINGIRA YA UPANDAJI KANISA | |
| **WATU WALIOMPOKEA YESU**<br>WAFUASI WA YESU | |
| **WATU WAPYA WALIOBATIZWA**<br>WATU WANAOSHIRIKI KATIKA SAKRAMENTI YA UBATIZO | |
| **VIONGOZI WAPYA WANAOENDELEA NA MAFUNZO**<br>WATU AMBAO MPANDA KANISA ANAWAFUNZA KWA AJILI YA UONGOZI | |

## VIKUNDI VIDOGO | Angalau wanafunzi wapya 2 na kiongozi 1

| | |
|---|---|
| **VIKUNDI VIDOGO VIPYA**<br>VIKUNDI VILIVYOANZISHWA MWEZI HUU | |
| **WASHIRIKI WAPYA KATIKA VIKUNDI VIDOGO**<br>WATU WAPYA WANAOSHIRIKI KATIKA VIKUNDI VIDOGO MWEZI HUU | |
| **VIONGOZI WAPYA KATIKA KIKUNDI**<br>VIONGOZI WAPYA KATIKA KIKUNDI CHINI YA UONGOZI WA MPANDA KANISA | |

## MAHITAJI YA KUOMBEA

1. ______________________________
2. ______________________________
3. ______________________________

## SHUHUDA

______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________
______________________________

# RIPOTI YA MAHAFALI

RIPOTI YA MWISHO

## TAARIFA YA JUMLA

| | |
|---|---|
| **MWEZI WA RIPOTI** | |
| **JINA LA MPANDA KANISA** | |
| **KANDA ANAYOTOKEA** | |
| **MRATIBU WA KANDA** | |

## TAARIFA ZA BINAFSI

| | |
|---|---|
| **WATU WAPYA ULIOWAFIKIA**<br>WATU ULIOWAFIKIA KATIKA MAZINGIRA YA UPANDAJI KANISA | |
| **WATU WALIOMPOKEA YESU**<br>WAFUASI WA YESU | |
| **WATU WAPYA WALIOBATIZWA**<br>WATU WANAOSHIRIKI KATIKA SAKRAMENTI YA UBATIZO | |
| **VIONGOZI WAPYA WANAOENDELEA NA MAFUNZO**<br>WATU AMBAO MPANDA KANISA ANAWAFUNZA KWA AJILI YA UONGOZI | |

## VIKUNDI VIDOGO | Angalau wanafunzi wapya 2 na kiongozi 1

| | |
|---|---|
| **VIKUNDI VIDOGO VIPYA**<br>VIKUNDI VILIVYOANZISHWA MWEZI HUU | |
| **WASHIRIKI WAPYA KATIKA VIKUNDI VIDOGO**<br>WATU WAPYA WANAOSHIRIKI KATIKA VIKUNDI VIDOGO MWEZI HUU | |
| **VIONGOZI WAPYA KATIKA KIKUNDI**<br>VIONGOZI WAPYA KATIKA KIKUNDI CHINI YA UONGOZI WA MPANDA KANISA | |

## KANISA JIPYA LILILOPANDWA

| | |
|---|---|
| **JINA LA KANISA JIPYA** | |
| **DHEHEBU**<br>KAMA LIPO | |
| **ANWANI**<br>UJIRANI \| JIJI \| JIMBO | |
| **TAREHE YA MAHAFALI** | |
| **IDADI YA WASHIRIKA** | |

**INAENDELEA UPANDE UNAOFUATA**

**MAHITAJI YA KUOMBEA**

1. ______________________________
2. ______________________________
3. ______________________________

**SHUHUDA**

Je, ni jinsi gani Mungu ametenda kazi kupitia kanisa hili jipya kusaidia kubadilisha maisha ya watu au jamii ambako kanisa limepandwa?

______________________________

Sahihi ya Mpanda Kanisa

________/ _____/ ______
Mwezi/Siku/Mwaka